# MITAZAMO KUHUSU KISWAHILI MIONGONI MWA WAZUNGUMZAJI WA KIJALUO: KIFANI CHA SHULE ZA MSINGI KATIKA KAUNTI YA MIGORI.

OWALA JAEL AKINYI

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

University of NAIROBI Library
0377598 8

NOVEMBA / 2014

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa popote kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu kingine chochote.

**Sahihi**……………………………… **Tarehe**…13/11/2014…

**JAEL AKINYI OWALA**

**(MTAHINIWA)**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

**Sahihi**……………………………… **Tarehe**…14/11/2014

**DAKTARI AYUB MUKHWANA**

**(MSIMAMIZI)**

**Sahihi**……………………………… **Tarehe**…14/11/14…

**DAKTARI JEFWA MWERI**

**(MSIMAMIZI)**

# TABARUKU

Ninaitabarukia kazi hii kwa familia yangu. Mume wangu mpendwa, Willis Okoth ambaye ameonyesha upendo wa dhati na kuwa mhimili wangu kwa hali na mali. Watoto wangu wawili Joy na Steve ambao wameonyesha uvumilivu mkubwa. Wazazi wangu marehemu Paul Owala na Lorna Owala ambao walinipa msukumo wa kujiendeleza kielimu.Mama, Mola akupe maisha marefu. Nawatabarukia kaka na dada zangu na hasa Christine ambaye alinipa msaada niliohitaji. Asante kwa mchango wenu. Mungu awabariki.

# SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati zinamwendea Maulana ambaye ameniwezesha kuikamilisha tasnifu hii, ambayo imekuwa na pandashuka zake. Kwa kweli alinipa nguvu, uwezo na neema ili niweze kuikamilisha safari hii.

Shukrani nyingi ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Ayub Mukhwana na Dkt. Jefwa Mweri. Walijitolea kwa hali na mali kunielekeza kila nilipowahitaji. Nashukuru kwa kuwa walikuwa na shughuli nyingi ila waliweza kunihudumia. Walinipa mawaidha na maelekezo ya kitaalamu ambayo yalinifaa sana. Kwa kweli nawaombea Mungu aweze kuwapa afya na awazidishie hekima na neema.

Nawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili ambao wamenielekeza katika kipindi cha usomi wangu hadi kufika katika kiwango cha Uzamili. Shukrani za dhati zimwendee Dkt. Raya Timammy ambaye amekuwa kielelezo kwangu tangu digrii ya kwanza, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Jefwa Mweri. Nawashukuru pia Prof. John Habwe na Prof. Kineene wa Mutiso.

Nawashukuru walimu wakuu walionisaidia kukusanya data. Namshukuru Mauko, Ouko, Ojwang' na Ogogo. Tasnifu hii haingekamilika bila mchango wenu.Aidha, nawashukuru wasomi wenzangu kwa ushirikiano wao katika masuala ya kiusomi na kijamii. Kwa kweli wamekuwa marafiki wa dhati kwa kunipa moyo. Hawa ni Ruth, Kisakwah, Vincent, Jane,Magdalene, Nyangeri, Sr. Teresia, Regina, Furaha, Miriam, Duncan, Tsuma, Mwangi, Muthoni, Margaret, Schola, Doris na Grace.

Familia yangu imechangia pakubwa ufanisi huu kwa hali na mali.Nawashukuru kaka na dada zangu, Christine, Willie, Sally, Leno, Dorry, Caro na Liz.Mola awabariki.
Nawashukuru Christine, Njeri na Joshua ambao wamenisaidia katika kuchapa tasnifu hii.
Mola awabariki kwa utu wema wao.
Sifa na utukufu kwa Mwenyezi Mungu.

## IKISIRI

Katika tasnifu hii, tumechunguza mitazamo kuhusu Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kijaluo kwa kurejelea shule za msingi katika Kaunti ya Migori. Madhumuni ya utafiti ni, kupambanua mitazamo kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi, walimu na wazazi wenye asili ya Kijaluo katika Kaunti ya Migori, kuchunguza mambo ambayo husababisha mitazamo tofauti tofauti katika Kaunti ya Migori miongoni mwa wanafunzi, walimu na wazazi kuhusiana na lugha ya Kiswahili na kuchunguza iwapo mitazamo hii ina athari katika matokeo ya mitihani ya Kitaifa ya darasa la nane katika somo la Kiswahili, katika Kaunti ya Migori. Mbinu tulizozitumia katika utafiti ni uchunguzi stahilifu na uchunguzi kiasi. Vilevile tulitumia hojaji, uchunguzi uelekezi pamoja na mahojiano. Maswali yaliyotumiwa katika hojaji yalikuwa maswali ya wazi, maswali funge na maswali ya viwango. Wanafunzi, walimu na wazazi walihojiwa ili kupambanua mitazamo yao katika lugha hii ya Kiswahili. Data ilichanganuliwa kwa kutumia baa grafu, majedwali ya frikwenzi pamoja na pai chati. Nadharia iliyotumiwa ilikuwa nadharia ya Saikolojia ya jamii. Matokeo ya utafiti yalikuwa kwamba, wanafunzi hufurika madarasani kwa hivyo hawashughulikiwi kwa njia inayofaa, walimu wana masomo mengi kupita kiasi kwa hivyo wamekosa motisha, watafitiwa wameathiriwa na lugha nyingine kama vile Kijaluo na Kiingereza. Mapendekezo yalikuwa kwamba, vifaa vya kufunzia na kujifunza kwa lughayaKiswahili viwe vya kutosha, walimu wa Kiswahili wanapaswa kuhudhuria warsha na kozi za kunoa ubongo, sera za shule kuhusu lugha zitumike kwa usawa, mandhari ya shule yasionyeshe mapendeleo, maingiliano kuhusu lugha ya Kiswahili yaimarishwe na mwisho Kiswahili kipewe hadhi kubwa kuliko lugha nyingine kama vile Kijaluo katika Kaunti ya Migori.

## YALIYOMO

UNGAMO ........ ii
TABARUKU ........ iii
SHUKRANI ........ iv
IKISIRI ........ v
YALIYOMO ........ vi

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........ 1**
1.1 Usuli wa Mada ........ 1
1.2 Tatizo la Utafiti ........ 2
1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 3
1.4 Haipothesia ........ 3
1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 3
1.6 Upeo na Mipaka ........ 5
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 6
1.8 Nadharia ya Utafiti ........ 10
1.9 Mbinu za Utafiti ........ 12
1.9.1 Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data ........ 13

**SURA YA PILI: MWINGILIANO KATIKA KUJIFUNZA LUGHA ........ 15**
2.1 Utangulizi ........ 15
2.2 Dhima ya Mwingiliano Katika Kujifunza Lugha ........ 15
2.3 Uhusiano Kati ya Lugha ya Kwanza na ya Pili Katika Kujifunza Lugha ........ 16
2.4 Ujifunzaji wa Lugha kwa Wanafunzi ........ 18
2.4.1 Viathiriwa Vinavyo Athiri Wanafunzi katika Ujifunzaji wa Lugha ya Pili ........ 19
2.4.2 Vipengee Tambuzi ........ 19
2.4.3 Vipengee Vinavyohusiana na Hisi ........ 20
2.4.4 Vipengee Vinavyohusu Akili na Vipaji ........ 20
2.4.5 Motisha na Mitazamo ........ 21
2.4.6 Nafsi ........ 22
2.4.7 Kipengee cha Kujistahi ........ 23

2.4.8 Athari za Nafsi Kuhusiana na Lugha ya Pili ....................24
2.5 Dhima ya Mafunzo Rasmi katika Kujifunza Lugha ....................24
2.5.1 Vipengee katika Mwingiliano Darasani ....................25
2.5.2 Uhusiano Kati ya Mwingiliano Darasani na Ujifunzaji wa Lugha ya Pili ....................26
2.6 Mazingira na Ujifunzaji ....................27
2.6.1 Mwingiliano Baina ya Mwanafunzi na Mazingira ya Ujifunzaji ....................27
2.6.2 Mazingira na Nafasi Katika Ujifunzaji wa Lugha ya Pili ....................28
2.7 Dhima ya Lugha Asili ....................29
2.7.1 Sera ya Lugha ....................30
2.8 Vipengele Visivyohusika na Lugha ....................30
2.8.1 Umbali wa Kijamii ....................31
2.8.2 Tofauti za Kiumri ....................32
2.8.3 Tofauti za Vipaji ....................33
2.8.4 Motisha ....................34
2.8.5 Mikakati katika Ujifunzaji wa Lugha ....................36
2.8.6 Kushawishika na Marika ....................38
2.8.7 Lugha inayotumika Kanisani ....................38
2.8.8 Viongozi ....................39
2.8.9 Hadhi ....................39
2.8.10 Ajira ....................39
2.9 Mitazamo ya Wanafunzi ....................39
2.10 Mitazamo ya Walimu ....................40
2.11 Mitazamo ya Wazazi ....................40
2.12 Hitimisho ....................41

**SURA YA TATU: VIPENGEE VINAVYOATHIRI MITAZAMO YA WAZUNGUMZAJI WA KIJALUO KWA LUGHA YA KISWAHILI ....................42**

3.1 Utangulizi ....................42
3.2 Watafitiwa katika Utafiti ....................42
3.2.1 Vipengee Visivyohusika na LughaVinavyoathiri Mitazamo Visivyo vya Kilugha44
3.2.2 Umbali wa Kijamii ....................44

3.2.3 Tofauti za Kiumri ........................................................................................................46
3.2.4 Tofauti za Vipaji........................................................................................................47
3.2.5 Motisha ........................................................................................................48
3.2.6 Elimu ........................................................................................................50
3.2.7 Kushawishiwa na Marika ........................................................................................................51
3.2.8 Lugha Inayotumika Kanisani........................................................................................................51
3.2.9 Viongozi ........................................................................................................53
3.2.10 Hadhi ........................................................................................................54
3.2.11 Ajira ........................................................................................................55
3.3 Muhtasari wa Vipengele Visivyohusu Lugha........................................................................................................56
3.3.1 Uchanganuzi wa Walengwa ........................................................................................................57
3.3.2 Umbali wa Kijamii ........................................................................................................58
3.3.3 Tofauti za Kiumri ........................................................................................................59
3.3.4 Tofauti za Vipaji........................................................................................................59
3.3.5 Motisha ........................................................................................................60
3.3.6 Elimu ........................................................................................................61
3.3.7 Kushawishiwa na Marika ........................................................................................................62
3.3.8 Lugha Inayotumika Kanisani........................................................................................................63
3.3.9 Viongozi ........................................................................................................64
3.3.10 Hadhi ........................................................................................................65
3.3.11 Ajira ........................................................................................................66
3.3.12 Hitimisho ........................................................................................................67

**SURA YA NNE: MATOKEO YA UTAFITI ........................................................................................................68**
4.1 Utangulizi........................................................................................................68
4.2 Umbali wa Kijamii........................................................................................................68
4.3 Tofauti za Kiumri........................................................................................................69
4.4 Tofauti za Vipaji ........................................................................................................70
4.5 Motisha ........................................................................................................70
4.6 Elimu........................................................................................................71
4.7 Kushawishiwa na Marika........................................................................................................72

4.8. Lugha Inayotumika Kanisani ........ 72
4.9 Viongozi ........ 72
4.10 Hadhi ........ 73
4.11 Ajira ........ 73
4.12 Hitimisho ........ 73

**SURA YA TANO: MUHTASARI NA MAPENDEKEZO ........ 74**
5.1 Utangulizi ........ 74
5.2 Muhtasari ........ 74
5.3 Hitimisho ........ 75
5.4 Mapendekezo ........ 76
MAREJELEO ........ 78

**VIAMBATISHO ........ i**
Kiambatisho cha Kwanza: Barua ya Kujitambulisha kwa Watafitiwa ........ i
Kiambatisho cha Pili: Hojaji kwa Walimu Wakuu ........ ii
Kiambatisho cha Tatu: Hojaji kwa Walimu ........ vi
Kiambatisho cha Nne: Maswali ya Viwango kwa Walimu wa KiswahilI ........ x
Kiambatisho cha Tano: Hojaji kwa Wanafunzi ........ xii
Kiambatisho cha Sita: Maswali ya Viwango kwa Wanafunzi ........ xv
Kiambatisho cha Saba: Hojaji kwa Wazazi ........ xvii
Kiambatisho cha Nane: Ratiba ya Wakati ........ xxii
Kiambatisho cha Tisa: Bajeti ya Tasnifu ........ xxiii

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Usuli wa Mada

Mzungumzaji binafsi ana umuhimu katika Isimujamii. Hii ni kwa sababu hakuna wazungumzaji wawili ambao wana lugha sawa, kwa vile hakuna wazungumzaji wawili walio na umilisi wa lugha ulio sawa. Tofauti baina ya wazungumzaji wenyewe huweza kuonekana tu panapo ubia lugha.Isitoshe, kila mzungumzaji ana sifa zake za kipekee.

Hudson,(1980)akimnukuu Robert Le Page (1968a) anasema kila mtu huunda mfumo wake wa mazungumzo ili ufanane na mazungumzo ya kundi fulani au makundi fulani ambayo angependa kujitambulisha kwayo.Yeye huitazama na kuchambua mifumo yao ya lugha.Motisha yake kwa kiasi kikubwa humshurutisha kuchagua na kubadilisha mazungumzo yake vilivyo.

Mitazamo ya watu kuhusu vitu au dhana fulani huweza kuwa na athari kwa vitu au watu hao. Hii ni kumaanisha kuwa,mitazamo ya watu kuhusu lugha huweza kuathiri namna watu huitazama lugha husika.Ni kwa misingi hii ambapo tunatafiti mitazamo kuhusu Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Dholuo, kifani cha shule za msingi katika Kaunti ya Migori. Kwa mujibu wa Katiba ya Kenya (2010) Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile lugha rasmi nchini Kenya.Jambo linalofanya utafiti huu kuwa muhimu.

Mathooko (2007) anasema lugha ya taifa ni lugha inayowakilisha jamii yenye watu wenye makabila tofauti kisiasa, kijamii na kitamaduni. Kwa hivyo; mbona lugha hii ya taifa isitumiwe kama inavyotarajiwa katika maeneo mengine humu nchini?

Lugha kwa ujumla hutumika katika asasi za utawala, siasa, sheria, biashara na elimu. Vyote hivi ni muhimu kwa maendeleo ya watu. Lugha huweza hata kuitambulisha jamii. Kwa mfano, watu wa kabila au jamii fulani hutumia lugha yao kama kitambulisho chao.Jinsi mtu anavyotumia lugha ya Kiswahili kwa mfano, huweza kumfichulia msikilizaji au msomaji mengi kuhusu eneo analotoka, jamii yake, taifa lake, kiwango chake cha elimu, umri, jinsia na hata muktadha wa mazungumzo. Katika hali hiyo, hiyo lugha pia humweka mtu katika kikundi fulani. Hivyo basi, lugha ina dhima ya kuitambulisha jamii na mtu binafsi. (Tazama Kimaro,H. katika Gazeti la Taifa leo Juni 29,2010).

## 1.2 **Tatizo la Utafiti**

Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile lugha rasmi nchini Kenya. Kutokana na hadhi hizi kilizopewa Kiswahili nchini Kenya, majukumu yake ni mengi.Mojawapo ni kuwaunganisha watu kutoka makabila au maeneo mbalimbali katika taifa la Kenya ili waweze kushirikiana na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya taifa lao.

Kaunti ya Migori ni kaunti ambayo ina wakazi kutoka sehemu nyingi . Kwa mfano, kuna wazungumzaji wa Suba-Dholuo,Wakuria,Waluhya,Wajaluo,Wasomali, Wahindi wachache Waarabu na Wanubi.Kutokana na mwingiliano huu wa jamaa mbalimbali, tungetarajia kwamba Kiswahili kingetumika zaidi katika maingiliano yao. Hata hivyo, uchunguzi wetu umeonyesha ya kwamba, lugha ya Kiswahili aghalabu haitumiwi kama inavyotarajiwa katika diskosi ya jamii na vilevile diskosi rasmi kama vile; katika mikutano shuleni,mahubiri makanisani na kwingineko.

Bila shaka kuna vikwamizi ambavyo huchangia hali kama hii kutokea. Vikwamizi vyenyewe ni pamoja na; umri, vipaji, motisha na mitazamo miongoni mwa vikwamizi vingine. Vikwamizi hivi huweza kusababisha matatizo kama vile matokeo duni katika mitihani ya Kiswahili.

## 1.3 **Madhumuni ya Utafiti**

Madhumuni ya utafiti huu ni:

1. Kupambanua mitazamo kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi,walimu na wazazi wenye asili ya Kijaluo katika Kaunti ya Migori.
2. Kuchunguza mambo ambayo husababisha mitazamo tofauti tofauti katika Kaunti ya Migori miongoni mwa wanafunzi,walimu na wazazi kuhusiana na lugha ya Kiswahili.
3. Kuchunguza iwapo mitazamo hii ina athari katika matokeo ya mitihani ya Kitaifa ya darasa la nane katika somo la Kiswahili, katika Kaunti ya Migori.

## 1.4 **Haipothesia**

1. Wanafunzi,walimu na wazazi wenye asili ya Kijaluo katika Kaunti ya Migori wana mitazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.
2. Mitazamo ya wanafunzi,walimu na wazazi kuhusu lugha ya Kiswahili katika Kaunti ya Migori husababishwa na mambo tofauti tofauti.
3. Matokeo ya Kitaifa ya darasa la nane katika somo la Kiswahili katika Kaunti ya Migori huathiriwa na mitazamo ya wanafunzi, walimu na wazazi.

## 1.5 **Umuhimu wa Utafiti**

Lugha ya Kiswahili ina dhima muhimu sana katika jamii ya Wakenya. Umuhimu wa lugha hii ya Kiswahili nchini Kenya unatushurutisha kama jamii kuchukua hatua za kuiimarisha na kuistawisha.Lugha hii ya Kiswahili inafaa ifundishiwe katika shule

zote nchini bila upendeleo kwani, lugha hii ya Kiswahili ina nafasi ya kipekee nchini na sote tunapaswa kuienzi.

Utafiti ulifanywa ili kuelewa hali halisia ya Kiswahili katika kaunti hii.Maswali tuliyouliza ni kama vile;

1. Lugha hii kwa mfano ilibainika kama huanzishwa kwa wakati gani kama lugha ya pili?
2. Wanafunzi hawa wana msingi thabiti katika lugha asilia nyumbani au hata shuleni?
3. Je, wanafunzi wanapata muda gani katika kusoma ili kujifunza lugha ya Kiswahili?
4. Lugha hii imefichuliwa kwao kupitia mikakati ipi?
5. Je, walimu wanafanya maandalizi mapema kabla ya kufunza somo lenyewe?

Kwa mujibu wa Buliba A. (2006) lugha ya taifa ina majukumu kadhaa kama vile: kuwaunganisha watu kutoka makabila au maeneo mbalimbali katika taifa ili waweze kushirikiana na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya taifa lao. Katika Kaunti ya Migori, kuna wakazi kutoka sehemu nyingi. Tunapowaangazia wazungumzaji wa Kiswahili wenye asili ya Kijaluo, tunapata ya kuwa mitazamo ya wanafunzi, marika shuleni, ujirani, na jamii kwa ujumla huweza kuwa na athari katika mchakato mzima wa kujifunza lugha ya pili. Athari zenyewe zikiwa aidha chanya au hasi. Tukapitikiwa akilini na maswali kama vile;

1. Je, lugha ya taifa inatumiwa vipi katika diskosi ya jamii na katika diskosi rasmi?
2. Je, ni mambo gani ambayo husababisha mitazamo tofauti tofauti miongoni mwa wazungumzaji wa lugha?

3. Je, mitazamo huathiri vipi kufunza na kufunzwa kwa lugha ya Kiswahili katika Kaunti ya Migori?

Kwa kuwa utafiti wetu ulifanywa katika shule za msingi, tulichunguza lugha inayotumika katika mikutano, katika ripoti za kila siku kwenye batli, maoni ya mwalimu mkuu kwenye batli hiyo, sera ya shule kuhusu lugha, ripoti zilizoandikwa na walimu walio zamuni, wito wa shule na mengineyo. Mambo haya yalitusaidia kuchunguza iwapo yaliyotajwa ni miongoni mwa vikwamizi vinavyopelekea mitazamo kuhusu Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kijaluo kuwa chanya au hasi.

Kwa mujibu wa Matundura, (2010), akimulika suala la Kiswahili na nafasi za ajira ulimwenguni, soko la Kiswahili limepanuka sana hasa ikichukuliwa kwamba lugha hii ni muhimu, sio Afrika Mashariki tu, bali ulimwenguni kote. Kuna mashirika mengi ya uchapishaji ambayo yanachipuka nchini na yanahitaji wahariri wa miswada katika kampuni hizo. Pia kutokana na kupanuka kwa sekta ya mawasiliano, kuna nafasi katika vyombo vya habari. Vyombo hivi huwahitaji wataalamu wa tafsiri na uhariri. Walimu wanahitajika katika shule za msingi, upili, vyuo vya walimu na vyuo vikuu ambavyo vinapanuliwa kila uchao. Bila shaka Kiswahili kina nafasi ya kipekee nchini na sote twapasa kukienzi. (Tazama Gazeti la Taifa Leo Januari 19, 2010).

### 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu kuhusu mitazamo miongoni mwa wazungumzaji wa Kijaluo kuihusu lugha ya Kiswahili, ulijikita tu katika jimbo dogo la Marindi. Marindi ni jimbo dogo linalopatikana katika Kaunti ndogo ya Suna Magharibi. Ijapokuwa kuna wazungumzaji wa Kijaluo katika maeneo mengine yanayopatikana katika kaunti hii ndogo, kama vile Oruba, Wasweta ya chini na Wasweta ya juu, uchunguzi wetu

kuhusu mitazamo ulifanywa tu katika jimbo dogo la Marindi. Jimbo hili lina shule nne za msingi. Utafiti ulihusu shule zote nne; Assar, Migori, Ragana na Nyanko kwa sababu shule hizi ni chache mno kuweza kufanyiwa sampuli ya kimaksudi.

Jimbo hili limeteuliwa kwa sababu linapatikana mjini Migori na lina wakazi kutoka sehemu nyingi. Kwa hivyo, itakuwa rahisi kufanya utafiti kupambanua ile hali halisia kuhusu mitazamo yao kuhusu lugha ya Kiswahili. Jimbo lenyewe litawakilisha yale yanayotendeka katika Kaunti nzima ya Migori.

Wakati wa kukusanya data tulikumbwa na upungufu kwa mfano, wengi wa watafitiwa hawakuzirudisha hojaji zao. Pia,kwa kuwa inabidi data irekodiwe na hatimaye ichanganuliwe, vifaa kama video vilihitajika. Vifaa vyenyewe ni ghali mno na wakati mwingine umeme uliweza kukosekana na kuathiri mchakato wa ukusanyaji na uchanganuzi. Pia uchapishaji wa hojaji zenyewe zilikuwa ghali mno kwani ilibidi ziwe za wanafunzi, wazazi, walimu wa Kiswahili na walimu wakuu na hojaji zile zililenga tu wale wanaojua kusoma na kuandika. Mwisho, wengi wa watafitiwa hawakuweza kujieleza kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili.

## 1.7 **Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Utafiti wenyewe unapewa msukumo na hali kwamba, lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na vile vile lugha rasmi nchini Kenya. Utafiti huu ulichunguza iwapo majukumu ya lugha hii yanatekelezwa hasa kupitia kwa kufunzwa shuleni. Katika Kaunti ya Migori kuna shule ambazo matokeo yake katika Kiswahili hayaridhishi kwa hivyo, maswali yaliyotupitikia akilini ni;

1. Mitazamo kuhusu lugha hii ya Kiswahili ni ipi?
2. Kwa nini matokeo ya mitihani ya Kiswahili hayaridhishi katika kaunti ya Migori.

3. Matokeo haya yana uhusiano gani na mitazamo?
4. Shida ni wanafunzi au walimu hasa wanaopatikana katika Kaunti hii ya Migori?

Suala hili la mwingiliano kuhusu lugha limeshughulikiwa na watafiti mbalimbali.Kwa mfano,Owiyo (2013) ambaye alitafiti kuhusu dhima ya mwingiliano baina ya lugha ya mama kwa jumla na lugha ya Kiswahili, na athari zake katika mtihani wa Kitaifa katika Kaunti ya Kisumu. Owiyo alitaja lugha ya mama kama kikwamizi kikuu katika kujifunza lugha ya pili. Mbali na haya mawazo yake, uchunguzi wangu ulipanuka kidogo na kuvisawiri vikwamizi kama vile, umri, vipaji, motisha na mitazamo. Pia nilijikita katika lugha ya Dholuo.

Vilevile Ogero, (2012) alitafiti vikwamizi vinavyopatikana shuleni na ambavyo huathiri matokeo katika lugha ya Kiswahili.Utafiti wake ulichunguza shule za upili katika Kaunti ya Kisii.Utafiti wangu uliegemezwa katika shule za msingi katika Kaunti ya Migori. Ogero alichunguza vifaa vinavyotumiwa shuleni na jinsi vifaa hivi vinavyoweza kuathiri matokeo. Pia alichunguza walimu na mitazamo yao kuihusu lugha ya Kiswahili.Hata ingawa mambo kuhusu mwingiliano na matokeo katika mitihani ya Kitaifa yalichunguzwa, suala kuhusu mitazamo lilipewa kipaumbele katika utafiti wangu.

Mitazamo kuhusu lugha imechunguzwa duniani mara nyingi ili kutimiza malengo mbalimbali. Hockett, (1958:8) anasema kwamba mitazamo kuhusu lugha huunda lugha ya mzungumzaji na vile vile hadhi ya lugha hiyo. Anasema, mitazamo huweza kuathiri kwa kina mategemeo ya baadaye ya lugha, ya nchi, ama jamii lugha fulani. Marko na Howard, (2003) waliangalia mitazamo ya lugha lakini wakajikita katika mitindo mbalimbali ya mazungumzo na lafudhi. Bradely, (2013) alizungumzia

mitazamo ya lugha akiegemea uhifadhi wake. Wanafunzi katika Chuo Kikuu Cha Maseno katika majarida yao pia walitoa michango yao kuhusu mitazamo ya lugha; kwa mfano, Ojwang, (2011) alizungumzia vizingiti vya kisiasa na vya Isimujamii ambavyo hukwaza upanuzi wa lugha nchini Kenya. Mwakarayz, (2011) anasisitiza kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Anataja kwamba mitazamo huathiri matokeo ya somo la Kiswahili katika shule mbalimbali. Anawataja wazazi kama kikwazo kikuu cha maendeleo ya somo hili na vile vile lugha ya Sheng'.

Katika kongomano la wasomi wenye nia ya kuimarisha hadhi ya lugha, kulikuwa na pendekezo kuwa Sheng' iharamishwe.Kongomano la chama cha wanafunzi wa Kiswahili Afrika Mashariki (CHAWAKAMA) lilipendekeza kwamba kijilugha cha Sheng' kikabiliwe ipasavyo kwa lengo la kuleta umoja na mshikamano wa taifa (Tazama Omwong'a Yabesh na Hugholin Kimaro katika Gazeti la Taifa Leo Machi 16, 2010).

Kiswahili kisiweze kupuuzwa na kipewe hadhi yake kama lugha yoyote ile. Matundura, (2010) anasema 'lugha ya taifa ina maadui wengi kuliko marafiki. Anamnukuu Habwe, (2010) anayedai kwamba Kiswahili sanifu katika vyombo vya habari kimo katika njia panda. Anasema kwamba Wakenya wanapaswa kuionea fahari lugha hii ya Kiswahili ambayo ina sheheni imani na tamaduni za Mwafrika. (Tazama Matundura, B. katika Gazeti la Taifa leo, Februari 5).

Watafiti wengine ambao wameshughulikia mitazamo ya lugha ni pamoja na Obura, (1982) ambaye alichunguza mitazamo na motisha, mikakati ya kujifunza lugha na mafanikio katika lugha ya Kifaransa katika shule za upili nchini Kenya. Aliorodhesha sifa kumi za mwanafunzi mwenye ufanisi. Uchunguzi wake ulihusu matokeo ya awali ya mitihani katika somo la Kifaransa.  Alitumia mfano wa hojaji ya Lambert na

Gardener, (1972) ambazo hutumiwa kwa wana umojalugha, uwililugha na traiglosia. Mukhwana, (2008) alilenga miji mikuu mitatu ya Kenya; Nairobi, Kisumu na Mombasa. Tatizo lake lilikuwa kwamba, mitazamo kuhusu lugha katika nchi za Afrika huangazwa kama kiini katika sera ya lugha, matumizi ya lugha na kujifunza kwa lugha. Utafiti wangu uliwiana na wake kwani sera hii ya lugha hutekeleza majukumu mbalimbali katika taifa. Nadharia aliyoitumia ilikuwa ya Saikolojia ya jamii. Utafiti wake uligundua kwamba mitazamo kuhusu lugha ya Kiswahili huathiriwa na umri wa watafitiwa.

Jambo jingine lilikuwa kwamba, watu wana uwezo wa kutumia lugha mbili zilizo tofauti kwa hivyo huwalazimisha watafiti kuwauliza wazungumzaji, upendeleo wao katika lugha husika na kutoa sababu za upendeleo ule. Tunapotafiti kuhusu mitazamo kuhusu Kiswahili, lazima wazungumzaji wawe na umilisi zaidi aidha katika Kijaluo ama katika lugha nyingine, na bila shaka kuwa na sababu za, aidha kufaidi utamaduni au kupanda ngazi kijamii.

Mbara, (2010) naye alitafiti kuhusu mitazamo ya lugha; ila alitafiti kuhusu mitazamo ya vijana kuhusu lugha ya Suba. Eneo lake la utafiti lilikuwa Kaksingri. Alitafiti kuhusu uwili lugha mfu. Aligundua kwamba lugha ya Suba ilikuwa imedondoshwa kama lugha asilia na wazungumzaji kuchukua ya Kijaluo. Nadharia aliyotumia ilikuwa ya Saikolojia ya jamii. Katika utafiti wake mwanasaikolojia wa jamii aliyemtaja alikuwa ni Lambert. Alitoa ufafanuzi wa Lambert kuhusu mitazamo ya lugha akisema kwamba mitazamo kuhusu lugha fulani huchukuliwa kama mitazamo kuhusu mzungumzaji wa lugha hiyo. Utafiti wake ulichunguza vijana na si watu wote katika eneo hilo.

Tafiti zote zilizotajwa hapo juu zina umuhimu kwa utafiti wangu. Tafiti hizi zote zimeegemezwa kwenye mitazamo kuhusu lugha; ila kuna pengo ambalo linahitaji kujazwa. Ingawa Mukhwana, (2008) ametafiti kuhusu lugha ya Kiswahili, utafiti wake haujachunguza lugha ya taifa kwa kina, pamoja na majukumu yake. Jambo la pili ni kuwa jamii iliyolengwa na utafiti wa sasa ni wa Wajaluo. Utafiti wa Mukhwana, (2008) umeangazia lugha ya Kiswahili kwa ujumla wake na kutaja miji mikubwa. Ni muhimu kuchunguza vile vile hali halisia kule mashinani. Ndiposa, utafiti wangu utafanywa katika jimbo dogo la Kaunti ya Migori kuwakilisha kaunti hiyo kwa ujumla wake. Utafiti unaofanywa katika shule za msingi hauwi na matokeo sawa na utafiti wa shule za upili. Lightbown, (2006) anasema kuwa ni jambo jema kutafitiwa kuhusu watu kuwa na uwili lugha katika utu udogo wao.

Suala hili la mitazamo kuhusu lugha ni suala ambalo lafaa lishughulikiwe vilivyo ndiposa nililitaja katika madhumuni yangu ya utafiti.Kwa kufanya hili, watafiti wengi sharti wachukue jukumu la kukuza lugha ili tuwe na ufanisi kwa ujumla. Serikali nayo yafaa iwe tayari kuchukua gharama ya kufanikisha mchakato mzima wa mitazamo kuhusu lugha. Mitazamo ikiwa chanya, wazungumzaji wa lugha kwa jumla, watasaidia kulisukuma gurudumu la ufanisi wa lugha na kwa muktadha huu Kiswahili. Matokeo yake yatakuwa ya kuinua viwango vya elimu katika asasi zote nchini.

## 1.8 **Nadharia ya Utafiti**

Nadharia itakayotumiwa na utafiti huu ni Nadharia ya Saikolojia ya jamii. Nadharia hii ni uchunguzi wa kisayansi kuhusu jinsi fikra za watu, hisia na tabia huathiriwa na waliowazingira. Ni utafiti wa kiujarabati. Kwa mujibu wa Lahey, (2011), nadharia ya Saikolojia ya jamii huchunguza jinsi watu binafsi huathiriana na wenzao.

Akimnukuu mwanasaikolojia wa jamii, Aronson, (1995), anasema ni lazima watu watagusane na wenzao ambao huwaathiri. Uchunguzi kuhusu mvuto, mahitaji na ushawishi si jambo la mjadala. Hatuwezi kumchunguza binadamu tu bila kuiangalia saikolojia yake katika muktadha wa kijamii na jinsi anavyoathiriwa katika muktadha wa kijamii. Katika uchunguzi uliokuwa ukifanywa kabla ya 1960 chukulizi kuhusu mitazamo ilikuwa duni na isiyo na uasili. Mawazo yaliyoenezwa kuhusu lugha hayakuwa ya kisayansi (Schiffman, 1976).

Saikolojia ya jamii inahusu vipengele ambavyo hutuongoza ili tuwe na tabia fulani hasa pale tulipo na wenzetu na huchunguza masharti ambayo husababisha tabia fulani au hata hisia fulani. Pia hupatanisha Saikolojia na Soshiolojia. Katika Saikolojia ya jamii mitazamo huelezwa kama tathmini yenye ujuzi wa kilimwengu inayomhusu mtu binafsi, kitu au mahali na ambayo huathiri fikra au utendaji. Wanasaikolojia wa jamii huchunguza jinsi mitazamo huundwa, muundo wa mitazamo, mabadiliko ya mitazamo na uhusiano baina ya mitazamo na tabia.

Waasisi wa nadharia ya Saikolojia ya jamii ni Lambert, (1963) pamoja na Gardner na Lambert, (1972) Lambert alipochapisha kazi yake, iliyohusu mitazamo kuhusu lugha katika shule moja ya uwili lugha kule Kanada, yeye na wenzake walibadilisha mifumo ya shule. Katika tafiti zao katika Chuo Kikuu Cha McGill, walitaja vipengele vikuu katika kujifunza lugha ngeni. Jambo la kwanza likiwa uwezo wa kufikiri, la pili, mtazamo mwafaka kuhusu lugha ngeni, pamoja na motisha katika kujifunza lugha hiyo ngeni.

Lambert na wenzake walipata ya kuwa wanafunzi wenye vipaji vya chini wanaweza kujifunza lugha ikiwa mitazamo yao kuhusu lugha hiyo ni chanya. Vilevile wale walio na mitazamo chanya wanaweza kujifunza lugha ikiwa vipaji vyao ni vya juu.

Walisema lazima tuwe na vipaji ili tujifunze lugha. Na tukiwa na mitazamo chanya, motisha na maelekezo ya mazingira, tunaweza kujifunza lugha geni kwa haraka zaidi.

Lambert na Gardner, (1972) walisisitiza kwamba, motisha kwa kiasi kikubwa husaidia kuleta ufanisi katika kujifunza lugha ya pili. Waligawa motisha kuwili; kwanza, haja ya mawasiliano na mitazamo kuhusu lugha geni. Walisema ya kwamba ikiwa wazungumzaji wanataka kufaidika kwa kupanda ngazi kijamii na kufaidi utamaduni, itawabidi wajifunze lugha ngeni. Kwa muktadha huu, Kiswahili kikifunzwa, kitatimiza majukumu ya taifa na wazungumzaji vilevile watakuwa na uwezo mkubwa katika mawasiliano yao ya kila siku.

Nadharia ya Saikolojia ya jamii itanisaidia katika kubainisha jinsi wanafunzi wanavyojifunza lugha ya pili na mambo ambayo huziathiri tabia zao hasa wanapojifunza lugha hii ya pili ambayo ni Kiswahili.

## 1.9 **Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ulichunguza Kaunti ya Migori kama kielelezo ili kubainisha mitazamo iliyopo kati ya Kiswahili na Kijaluo. Kifani kilitumiwa ili kujibu maswali ya kwa nini? au vipi? Maswali haya ni yale ambayo mtafiti hana uwezo wa kuyadhibiti. Punch, (2011) akimnukuu Goode na Hatt, (1952: 331) anasema kifani ni njia ya kupanga data ya jamii ili kuhifadhi sifa za umoja kuhusu kile kinachochunguzwa. Akimnukuu Miles na Huberman (1994), anataja kifani kama mtu binafsi, kikundi cha watu, shirika, jamii ama taifa.

Mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu ni pamoja na; uchunguzi elekezi, hojaji, mahojiano na uelekezi na elekevu wa kutambua. Kwa kiasi kikubwa uchunguzi huu ulipatadata nyingi kutoka kwa uchunguzi uelekezi. Hojaji zilitumiwa ili kumwelekeza

mtafiti hasa anapouendeleza utafiti wake nyanjani. Mbinu kama mahojiano ya ana kwa ana na ya simu yangesaidia katika kuendeleza utafiti. Watafitiwa walitoa kauli zao kuhusu mitazamo yao ya lugha. Walimu wawili kutoka katika kila shule walihojiwa. Katika utafiti wenyewe maswali yaliyoulizwa yalikuwa ya wazi, ili mhojiwa apate nafasi ya kutoa maoni yake. Kulikuwa na maswali ya viwango ambayo yaliulizwa kukadiri mitazamo ya mhojiwa hasa anapofafanua anavyokubaliana au kutokubaliana na taarifa fulani. Mwisho kulikuwa na maswali funge ambayo yalijumuisha kwa mfano maswali yenye hiari mbili. Wanafunzi sita katika kila shule walihojiwa, wakiwa wasichana watatu na wavulana watatu katika kila shule. Wazazi pia walihojiwa kwa muda wa dakika kumi makazini mwao.

### 1.9.1 Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Punch, (2011) data ni habari inayoweza kuchunguzwa kuhusu ulimwengu. Mugenda et al (1999) wanaeleza data kama habari zote ambazo mtafiti anakusanya ili zimsaidie katika utafiti wake. Wanaainisha data kuwili; data msingi na data sekondari. Wanafafanua data msingi kama habari ambazo mtafiti anapata nyanjani. Data sekondari inaelezwa kama habari ambazo mtafiti anatoa kwenye vitabu, nakala na majarida, yaani maktabani.

Utafiti huu ulifanywa kwa awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa pale ambapo mtafiti alijifahamisha na yaliyoandikwa maktabani kuhusu mitazamo ya lugha. Kwahivyo alisoma vitabu, magazeti, majarida na vijarida. Sababu ya kusoma ni kupata ufahamu kuhusu yale yote ambayo yameandikwa kuhusu mada yake.Utafiti ulitumia hojaji, mahojiano, majadiliano na uelekevu wa kutambua. Awamu hii, ilimsaidia mtafiti aweze kuteua wahojiwa na vilevile kuandaa maswali atakayouliza kupitia kwa mbinu mbalimbali.

Jimbo letu dogo la utafiti liliwakilisha Kaunti nzima ya Migori. Hii ni kwa sababu utafiti haukuwa na muda wa kutosha wa kuchunguza Kaunti nzima ya Migori. Isitoshe, utafiti kama huo ungeweza kuwa na gharama ya juu.Awamu ya pili ilikuwa ya mahojianoyenyewe. Mahojiano yenyewe yalifanywa katika shule hizo nne,ofisini na katika makazi. Utafiti katika makazi ulichukua muda wa dakika kumi kwa kila mhojiwa, ili wawe na muda wa kutosha wa kuyajibu maswali yote. Wale waliohojiwa ni wenye umri kati ya 18 na 35. Hawa ni watu wazima ambao wana uwezo wa kujieleza na kutoa taarifa kamili kuhusu mitazamo yao ya lugha kupitia kwa majadiliano.

Mahojiano yalifanywa ana kwa ana nyanjani, ili mtafiti aweze kupata maelezo kwa kina. Umuhimu wa mahojiano ni kumwezesha mtafiti kupata mambo ambayo hayawezi kuchunguzwa kwa uwazi kama vile fikra, mitazamo, hisia na mengineo. Mhoji aliweza kutumia ujuzi wake kumfanya mhojiwa atoe fafanuzi, hasa kutoka kwa wale wahojiwa wanyamavu. Mhoji alipata tabia za kibinafsi za wale wahojiwa.Majibu yale yalirekodiwa kwa kutumia aidha kinasa sauti au kwa maandishi. Majibu yale yalitolewa kwa kutumia majedwali ya frikwenzi.Viathiriwa vilihusu umri, jinsia, makazi na viwango vya elimu. Mbinu hii ilitusaidia katika uchanganuzi wa data yetu na hata katika utoaji wa mahitimisho.

# SURA YA PILI

## MWINGILIANO KATIKA KUJIFUNZA LUGHA

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia kwa jumla suala la dhima ya mwingiliano katika kujifunza lugha, ili iwe kama mhimili wa yale tutakayosema baadaye kuhusu mada yetu ya utafiti.Suala hili linajadiliwa kwa sababu bila uelewa tosha wa mwingiliano kama dhana ya Isimujamii, ni vigumu kujadili mitazamo ya wanajamii hasa katika maingiliano ya lugha.

### 2.2 **Dhima ya Mwingiliano Katika Kujifunza Lugha**

Mwingiliano umevutia shauku kubwa katika ujifunzaji wa lugha ya pili katika muongo uliopita.Long(1990) alipendekeza kuwa mwingiliano ni muhimu kwani hukuza ujifunzaji wa lugha ya pili.Anaitetea kauli hii kwa kusema kwamba mwingiliano ina vipengee vitatu: pembejeo, uzalishaji na mwitiko.Pembejeo ni lugha inayowasilishwa kwa anayefunzwa lugha na wazungumzaji asili au wazungumzaji wengine.Wazungumzaji wa lugha ya pili hutumia pembejeo hii ili kuiundia haipothesia.Uzalishaji nilugha inayozungumzwa na wazungumzaji wenyewe wanaojifunza lugha.Mwitiko kwa upande mwingine ni athari inayotokana na wale washirikishi wa uzalishaji wa lugha inayofunzwa.

Kwa hivyo wazungumzaji wa Kijaluo wanapoingiliana na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili katika muktadha wa kujifunza lugha, bila shaka watajifunza lugha ya pili ambayo ni lugha ya Kiswahili.Ujifunzaji wao wa lugha ya pili, utakuwa na athari mbalimbali zitakazotokana na kujifunza huku kwa lugha hiyo ya pili.Haya ni mambo ambayo tutakumbana nayo baadaye katika utafiti wetu.

## 2.3 Uhusiano Kati ya Lugha ya Kwanza na ya Pili Katika Kujifunza Lugha

| | **LUGHA YA KWANZA** | **LUGHA YA PILI** |
|---|---|---|
| UFANISI WA LUGHA | Watoto huwa na ustadi kamili wa lugha ya kwanza. | Wazungumzaji wa lugha ya pili walio na umri mkubwa hukosa ustadi kamili. |
| MALENGO | Umilisi katika lugha lengwa | Wazungumzaji wanaojifunza lugha ya pili hawana umilisi na usahihi katika lugha lengwa ila hujibiidisha na usanifu kwa ujumla wa lugha ya pili. |
| UWEZO WA KUELEWA | Watoto hukuza uwezo wa usahihi. | Wazungumzaji wanaojifunza lugha ya pili wakati mwinginehushindwa kufanya maamuzi yanayozingatia sarufi. |
| USHAHIDI HASI | Marekebisho hayapatikani wala hayahitajiki. | Huwa na dhima kuu hasa katika kubainisha ustadi. |

Kwa ujumla tofauti moja kati ya ujifunzaji wa lugha ya kwanza na ya pili ni kuwa mchakato wa ujifunzaji wa lugha ya pili huathiriwa na lugha ambazo mzungumzaji tayari anazitambua. Hii hujulikana kama kuhamishwa kwa lugha. Uhamisho huu wa lugha sio lazima uwe kutoka kwa lugha asili.Huweza kutoka hata kwa lugha ya pili au hata ya tatu.

Ujifunzaji wa lugha ya kwanza huendelezwa kwa kusikiliza wale waliotuzingira, mazungumzo yao na hata jinsi sentensi zao zilivyoundwa.Kabla hata ya kusoma au hata kuliandika neno moja katika lugha ya kwanza, tunatumia misamiati na miundo muhimu ya sarufi.Wazungumzaji wengine hawapati hata muda wa kujifunza kusoma na kuandika na bado wana uwezo wa kujifunza lugha ya kwanza kwa usanifu.

Ujifunzaji wa lugha ya pili ni mchakato tendi sio kama wa lugha ya kwanza. Ujifunzaji wa lugha ya pili ni mchakato tendi, kwani ni sharti tujifunze misamiati na vilevile sarufi ili kufikia malengo yetu. Ujifunzaji huu huhitaji waelekezi, au kuelekezwa kutoka kwa vitabu fulani ama hata kutokana kwa kozi ya kusikia.Ujifunzaji huu huhitaji miaka mingi ya masomo au hata kuishi kwa muda katika nchi fulani. Wazungumzaji wengi hawafikishi malengo yao ya usanifu katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Chomsky, (1969) anasema kuwa watoto wote hujaliwa na sarufi bia inayohusu kanuni ambazo ni bia na kwamba, lugha zote za wanadamu ni uzao wa wazungumzaji wa lugha husika ambao huzingatia kanuni zile zile. McLaughlin, (1972) akihakiki maoni ya wenzake anasema kwamba hakuna kuhamishwa kwa lugha kwa watoto wanaojifunza lugha ya pili ila pale ambapo mtoto huyu atatengwa na marika wa ile lugha lengwa.

Msimamo wangu ni kuwa watoto wote hupata lugha ya kwanza na hata ya pili kwa sambamba.Watoto huanza kwa kuzungumza kama wazazi wao lakini mara tu wanapotagusana na marika zao huanza kuzungumza kama wale marika zao.Watoto kama hao hujichagulia lugha na sarufi na hata kubuni kanuni zao.Katika mazingira yao, watoto hao hujiendeleza kimwili na vile vile kiakili.Watoto hao huchuja mambo ambayo kwao yanaonekana tata na kurekebisha yale ambayo yatawafaidi.Kwa hivyo

watoto hawapati ama kujifunza lugha tu kwa kuiga kikasuku bali kwa ushahidi chanya wa yale waliyoyasikia.

Ujifunzaji wa lugha ya pili hujulikana kama uigaji wa jinsi wazungumzaji asili hujifunza lugha yao ya kwanza. Kama mwelekezi yeyote yule, ni sharti uwaelewe wanafunzi wako ili uridhishwe na uwezo wao. Ila iwapo kutaonekana kama kuna makosa yoyote uweze kutumia mikakati mwafaka ili uweze kuyarekebisha makosa haya vilivyo.

## 2.4 Ujifunzaji wa Lugha kwa Wanafunzi

Katika ujifunzaji wa lugha ya pili, lugha ya kipekee ambayo wanafunzi huelekezwa kwayo ni ile ya darasani.Lugha yao hutoka kwa walimu wao, kwa vifaa na kwa wanafunzi wengine.Lugha ya walimu wao huwa na mipaka.Vilevile lugha baina yao na wanafunzi wengine pia huwa na mipaka na hujaa makosa chungu nzima.

Ellis, (1985) anasema wanafunzi wanaojifunza lugha darasani huwa na uelewa mkubwa wa lugha husika kuliko wale wasiojifunza darasani. Rubin, (1975) anataja sifa kadhaa za mwanafunzi stadi wa lugha. Kwanza anashawishika na elimumwendo ya wanakikundi wakati wa mafunzo ili asiweze kupatwa na dukuduku hasi na ujizuiaji. Hivi wataweza kutumia nafasi zote kwa kujifunza lugha lengwa. Pia atumie nafasi zote katika kujizoesha kusikiliza na kujibu mazungumzo yoyote yanayoelekezwa kwake na kwa wenzake. Mzungumzaji huyu atakuwa na shauku kubwa ya kujifunza lugha ya pili na kuwa na motisha katika majukumu yote anayopaswa kuyatekeleza.Lazima awe tayari kuthubutu, kujifunza lugha husika hata kama itamfanya aonekane mjinga.Awe tayari kufanya marekebisho yoyote yanayohusu mambo ya lugha hiyo husika.

### 2.4.1 Viathiriwa Vinavyo Athiri Wanafunzi katika Ujifunzaji wa Lugha ya Pili

Kwa mujibu wa Ellis,(1985)viathiriwa hivyo ni kama vile vipengee tambuzi na vile vinavyohusiana na hisi za watu, vinavyohusu akili,vipaji, nafsi, motisha na mitazamo na mapendeleo ya wanafunzi, imani ya wanafunzi na umri wao.

### 2.4.2 Vipengee Tambuzi

Tofauti moja baina ya mtoto mdogo na kijana au mtu mzima ni uwezo wa kijana kutambua lugha akiwa darasani. Watu wazima wanaojifunza lugha huweza kujifunza wakizingatia zile kanuni za isimu. Kila wanapotumia lugha huzingatia kanuni zenyewe. Watoto kwa upande mwingine hutumia lugha kitabia kwa kuzingatia maana yake.

Ellis, (1985) akimnukuu Halliday, (1973) anasema kuwa mtoto mdogo hatilii maanane maelezo ya lugha ni nini,bali hutambua dhima ya lugha yenyewe. Rosansky, (1975) anaamini kuwa kujifunza kwa lugha ya pili huweza kutokea kwa njia mbili: kwamba mwanafunzi yule hutambua yale anayoyafanya. Yeye hujiamini tu na hatambui kwamba anajifunza lugha. Hana mitazamo tofauti tofauti kati ya lugha moja akilinganisha na nyingine. Mwanafunzi huyu huwa tayari kujifunza lugha nyingine.

Watu wazima kwa upande mwingine hawawezi kujifunza lugha bila kutambua kwamba wanajifunza. Wao huwa na mitazamo tofauti tofauti kuhusu lugha yao wenyewe pamoja na lugha lengwa. Jambo hili huweza kuwa kizuizi katika kujifunza lugha hiyo ya pili.

Rosansky (ibid) anasema kuwa ni utambuzi huu ambao unaletwa na umri ndio unaozuia kule kujifunza lugha kiasili na kusababisha uchaguzi tofauti. Anasema pia kuwa jambo ambalo hufanya vijana kujifunza lugha vyema zaidi kuliko watu wazima ni hali yao ya kumbukumbu.

### 2.4.3 Vipengee Vinavyohusiana na Hisi

Brown, (1980b) anaonelea ya kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili huhusishwa na uzoeaji wa utamaduni. Anataja vipengee vinne vya uzoeaji wa utamaduni.Kwanza ni sisimko la awali na hali ya kuwa vinahusiana na hisi na kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Pili ni mashambulizi ya kiutamaduni ambayo husababisha ile hali ya kutenganishwa na kutokubali lugha lengwa. Tatu ni uzito wa kiutamaduni, usimilishaji na kukubali tamaduni ngeni. Anataja kipengee cha tatu kama kilicho muhimu zaidi ya vyote katika kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili.Watoto hawajahusishwa sana na mambo ya utamaduni kama vile watu wazima. Kwa hivyo wao hujifunza lugha ya pili haraka zaidi kuliko watu wazima.

Neufeld, (1978) anahakiki mawazo ya Rosansky, (1975) na kusema kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili hauathiriwi na mambo ya umri.Neufeld anasema kwamba watoto hupata msukumo zaidi kutokana na motisha ya lugha ya asili na kwa hivyo aghalabu hujikita zaidi kwenye matamshi na hata lafudhi inayotokana na lugha ya asili.

### 2.4.4 Vipengee Vinavyohusu Akili na Vipaji

Vipengele hivi vinahusu ule uwezo wa kuwa stadi na vilevile kuzitumia mbinu za kitaaluma katika kujifunza lugha ya pili. Oller na wengine, (1978), wanasema kipengee hiki kinachohusu akili si kipengee cha lazima katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ellis, (1985) anasema uwezo wa kiakili huweza kuathiri kujifunzwa kwa mbinu nyingine ambazo huhusishwa na ujifunzaji wa lugha ya pili, ila hauwezi ukaathiri

uwezo wa kujifunza mbinu za kuzungumza kwa usanifu. Anasema kuwa uwezo huu wa akili huweza kumfanikisha mwanafunzi anayepokea masomo yake darasani.

Kwa upande mwingine, vipaji kwa mujibu wa Caroll na wengine, (1959) haviwezi kukadiriwa vikihusishwa na tabia. Wataalamu hawa wanakariri kwamba vipaji vina vipengee vyake vilivyo muhimu katika kujifunza lugha ya pili. Vipengee hivi vina athari muhimu katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwani huzingatia zaidi viwango vya ustadi vinavyotimizwa na wanafunzi darasani. Naye Gardner, (1980) anapendekeza kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya vipaji na ustadi katika kujifunza lugha ya pili. Krashen, (1981a) anatofautisha mambo mawili kuhusiana na ujifunzaji lugha ya pili; kupata ujuzi na kujifunza. Anasema kuwa vipaji huhusisha kule kupata ujuzi ambao huweza kupatikana tu darasani.Anasema kwamba vipaji aghalabu huweza kuhusishwa na umri, na huweza kuathiri ufanisi katika ujifunzaji wa lugha ya pili, hasa inapokadiriwa kwa kutumia mitihani darasani na inayohusu uwezo wa kiisimu.

**2.4.5 Motisha na Mitazamo**

Ellis, (1985) anasema kuwa tabia ya mzungumzaji hudhibitiwa na mahitaji yake pamoja na mapendeleo yake, mambo ambayo huathiri jinsi anavyotekeleza wajibu wake. Schumann, (1978)anataja mitazamo kama kipengee cha jamii. Anaihusisha mitazamo na viathiriwa kama vile motisha pamoja na ukubwa wa kikundi kinachofunzwa lugha ya pili.

Gardner na Lambert (1972), wanataja motisha kama malengo ya kijumla ya mwanafunzi wa lugha ya pili na vilevile mitazamo kama msimamo wa mwanafunzi katika kufikia malengo yake ya ujifunzaji lugha ya pili. Gardner, (1979) anasema kuwa mitazamo huhusishwa na motisha kwani hutegemeza maelekezo ya mazingira kwa mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili.

Gardner na Lambert (1972), wanatambua motisha kuwa jinsi mwanafunzi wa lugha ya pili anavyohitaji kujitambulisha na utamaduni wa lugha ya pili. Wanachangia mawazo ya Mowrer (1960), ambaye anazungumzia ujifunzaji wa lugha ya kwanza. Mowrer anaeleza kwamba mtoto hujihusisha na lugha anayosikia hasa ikiwa ni ya wazazi wake. Kwa hivyo jinsi mtoto huyu anavyojitambulisha na lugha ya wazazi wake, ndivyo anayejifunza lugha ya pili anavyopata motisha ya kujihusisha na lugha hiyo ya pili kwa kujifunza lugha yao.

Gardner na Lambert (ibid), wamebainisha mitazamo inayohusu lugha ya pili. Stern (1983), naye anataja vipengee vitatu. Moja, mitazamo kuhusu jamii-lugha, cha pili, mitazamo kuhusu kujifunza lugha hiyo ya pili, na tatu ni mitazamo kuhusu lugha na ujifunzaji wa lugha kwa jumla.

Kwa ujumla, Gardner na Lambert (1980), wana maoni tofauti tofauti kuhusu motisha na mitazamo ya ujifunzaji lugha ya pili.Wanasema kwamba motisha na mitazamo ni vipengee muhimu ambavyo husaidia kuitambua viwango vya ustadi vinvyotimizwa na wanafunzi tofauti tofauti wanaojifunza lugha ya pili. Wanaeleza kwamba wanafunzi wenye ufanisi mkubwa ni wale ambao wana vipaji na viwango vya juu vya motisha kuhusiana na ujifunzaji wa lugha. Ellis (1985), anapohakiki mawazo ya akina Gardner, anasema kwamba si rahisi kutambua iwapo motisha ndio husababisha ufanisi katika kupata ujuzi wa lugha ya pili na kwamba kupata ujuzi ndio huboresha motisha.

### 2.4.6 Nafsi

Nafsi hutazamwa kama kipengee ambacho ni muhimu katika kufaulu au kutofaulu kwa mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili. Katika kipengee cha nafsi, kuna vipengee vingine vidogo vinavyohusu usondani na undani. Watafiti wengi

wametafitia ule uhusiano baina ya usondani na undani na kupendekeza kwamba, mambo haya huathiri utendaji wa mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili.

Kwa mujibu wa Eysenck na Eysenck (1964), msondani ni mtu ambaye ni mchangamfu, ambaye hushirikiana na watu wengi, na huthubutu katika mambo yake, ilhali mndani ni mpole, anayechangamkia vitabu vyake kuliko watu wengine, asiyeonyesha hisia zake kwa urahisi.

Wengi wa wananadharia wa lugha ya pili wanadai kwamba wasondani wengi ni wanafunzi stadi wa lugha. Cook (1991), anasema kwamba wasondani hao huchangia katika mazungumzo ndani ya darasa, ilhali Swain (1985), anasema kwamba wasondani hawa huchangia katika mazungumzo hata katika mazingira yanayopatikana nje ya darasa. Wao hutumia kila nafasi wanayoipata kuitumia lugha hiyo ya pili. Pia huwasiliana na wazungumzaji wengine wa lugha ya pili, kwa hivyo wana mwingiliano mkubwa. Hawaogopi kuthubutu kila wanapopata nafasi na hujaribu kuzungumzia aina ya maneno na hata miundo ya sarufi kwa hali ya juu kimazungumzo.

### 2.4.7 Kipengee cha Kujistahi

Hiki ni kipengee ambacho mtu binafsi hujiona kwamba ana thamani kwa mfano huweza kujiona kama mtu mwenye ustadi au mtu asiye na ustadi. Mtu anayejistahi huonyesha katika tabia yake kwa mfano, kuwa na uwezo na kujigamba.

Holly (1987), anasema kuwa utafiti unaoonyesha ya kwamba mwanafunzi ambaye anajihisi kujistahi kwa kiasi kikubwa huweza kupata ufanisi. Andres (1993, 1996), anasema sifa hii ya kujistahi huweza kugeuzwa na kuboreshwa katika darasa ambalo lugha ya pili inafunzwa ili matokeo yawe ya kufana katika ufunzaji wa lugha ya pili.

Aghalabu viathiriwa ambavyo hutafitiwa hapa ni ufasaha, usahihi na uchangamano. Wanafunzi wasondani huweza kuwa na ufasaha katika mazungumzo yao ya lugha ya pili.

### 2.4.8 Athari za Nafsi Kuhusiana na Lugha ya Pili

Nafsi huhusiana kwa ujumla na ujifunzaji wa lugha ya pili. Kwa mujibu wa kipengee hiki, wanafunzi wana uwezo wa kujiamini, wana kiwango cha kuhisi maono ya wengine na kwa kiwango kikubwa uwezo wa kuchanganua mambo. Wanafunzi hawa huchukua muda wao mwingi katika kusikiliza yale yanayosemwa na wenzao na kukatiliwa tamaa na mambo kuhusu makosa yao katika mawasiliano.

## 2.5 Dhima ya Mafunzo Rasmi katika Kujifunza Lugha

Kwa mujibu wa Ellis (1994), mafunzo rasmi husaidia utafiti wa lugha ya pili kwa vipengee vitatu. Kipengee cha kwanza kinahusu tafiti linganishi. Utafiti huu huangalia mbinu tofauti tofauti za kufunza na kujifunza lugha ya pili. Kipengee hiki hakihusishi muktadha wa darasa kwa njia yoyote ile. Kipengee cha pili ni kile cha muktadha wa darasa. Kipengee hiki huangalia darasa kama eneo ambalo kwalo, miingiliano mbalimbali hutokea. Miingiliano hii husaidia katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwa wanafunzi.

Wright (1984) naye, kufungamana na ujifunzaji wa lugha ya pili, anasema mambo yote ambayo yanatendeka darasani yanasababishwa na mwingiliano halisi wa mzungumzaji mmoja na mwingine.Kipengee cha tatu ni kutafiti athari za mafunzo rasmi kwa ujifunzaji wa lugha ya pili. Swali ambalo linajitokeza hapa ni; je, wanafunzi hunufaika vipi na yale ambayo wanafunzwa?

### 2.5.1 Vipengee katika Mwingiliano Darasani

Mwingiliano darasani huhusishwa na mwingiliano kati ya walimu na wanafunzi na kati ya wanafunzi wenyewe. Mwingiliano kati ya walimu na wanafunzi kwa mujibu wa Long na Sato (1983) ni miingiliano ambayo huhusishwa na kurekebishwa kwa makosa, maelezo ya mwalimu na majibu ya mwanafunzi kwa mwalimu wake.Nao Allwright na Bailey (1991) wanaonyesha ya kwamba walimu huandaa masomo yao kwa kujiegemeza kwenye silabasi, mbinu na mazingira ya ufunzaji. Maandalizi yao huzua miingiliano darasani. Wanafunzi huchangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha miingiliano hii. Miingiliano darasani itafanikishwa kwa kuzingatia miundo na sifa ambazo zinahusu mawasiliano baina ya wanafunzi na mwalimu. Pia kuna matumizi ya lugha. Allwright (1990) anataja mifano kama vile sampuli yaani madhihirisho ya lugha lengwa, maelekezo kuhusu mawasiliano juu ya lugha lengwa na utendaji katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Tunapoangazia marekebisho ya mwalimu kwa mwanafunzi, tunapata kuwa wanafunzi wengi hufanya makosa hasa wanapojifunza lugha ya pili. Jambo hili laweza kuwa kipengee kinachosaidia katika kujifunza lugha ya pili.Wanafunzi wengi pamoja na walimu wao huhisi ya kuwa ni mojawapo ya majukumu ya mwalimu kuwaarifu wanafunzi hasa wanapotenda makosa katika kujifunza lugha ya pili.

Mwingiliano kati ya mwanafunzi mmoja na mwingine huhusu wanafunzi wawili au hata kundi zima katika kujifunza lugha ya pili.Miingiliano hii husaidia katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Tafiti zadai kwamba wanafunzi wanaofanya kazi kwa makundi huwa na matokeo mazuri katika mitihani yao na vile vile sifa ya juu ya kujistahi. Stahl, (1995) anasema wengi katika wanafunzi hawa huweza kutambua yaliyomo kuhusu mbinu wanazozisoma katika kujifunza lugha ya pili.

### 2.5.2 Uhusiano Kati ya Mwingiliano Darasani na Ujifunzaji wa Lugha ya Pili

Kwa mujibu wa Krashen (1982), Swain (1985) na Prabhu (1987), njia bora zaidi ya kufaulisha umilisi wa lugha ya pili darasani ni kwa wanafunzi kuchangia katika mawasiliano yao madarasani. Wong Fillmore (1982) naye anasema kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili darasani ulio na ufanisi ni ule ambao huwapa wanafunzi wengi ujuzi wa lugha ya pili na wanapata maelekezo yao kutoka kwa walimu. Anasema kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili hauwezi kufaulu katika darasa ambalo wanafunzi hutumia muda wao mwingi wakiwasiliana na wanafunzi wenzao aghalabu katika lugha yao ya kwanza ama pale ambapo lugha wanayoelekezwa kwayo si sanifu.

Wong Fillmore, (1985) anatambua vipengee ambavyo tafiti za madarasa sitini zimependekeza. Amezigawa tafiti zake kuwili. Kwanza ni kuhusu mipangilio darasani, na sifa ya mazungumzo ya mwalimu. Anapendekeza kwamba madarasa ambayo yanafaulu katika ujifunzaji wa lugha ya pili ni yale ambayo hupata maelekezo yao kutoka kwa mwalimu, ilhali yale ambayo wanafunzi hujielekeza hayafaulu. Ni sharti wanafunzi wenyewe wapokee mafunzo rasmi. Mwalimu wao awe stadi na aweze kuuwasilisha ujumbe wake kwa njia mwafaka. Asijirudie rudie bali awe na ufasaha katika lugha yake. Pili, Long (1990b) anapohakiki mawazo ya wananadharia wa awali anasema kwamba mambo haya hayawezi kutumiwa kikamilifu na walimu kwani, tafiti zinahusu viwango vidogo, na pia athari za siku za usoni hazikujadiliwa kwa kina.

Msimamo wangu ni kwamba walimu wanapaswa kutumia maono chanya kuhusu wanafunzi wao na pia wakizingatia madarasa yao katika kufunza lugha ya pili. Kwa mfano, waweze kujiuliza kwamba, ni viathiriwa vipi ambavyo vikitumiwa darasani vitafaulisha ujifunzaji wa lugha ya pili?

## 2.6 Mazingira na Ujifunzaji

Mazingira yanahusu jamii, vipengee vya kitamaduni, vipengee vya kisaikolojia na mazingira kwa ujumla. Mazingira huwabadilisha wanafunzi kitabia na vilevile wanafunzi wenyewe huathiri mazingira yao.

### 2.6.1 Mwingiliano Baina ya Mwanafunzi na Mazingira ya Ujifunzaji

Mazingira ya ujifunzaji yanaweza kuhusu mwanafunzi, wanafunzi wengine, walimu na mazingira yake kwa ujumla. Earthman, (2004), anataja kuwa ubora wa mazingira ya mwanafunzi huathiri uwezo wake na jinsi anavyojifunza.Earthman anasema kwamba mazingira yenyewe ni sharti yawe ya kirafiki, malango yawe yanayokubalika, na walimu wawajibike vilivyo. Tafiti zingine zasema kwamba majengo mabaya husababisha matokeo mabaya kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili.

Bunting, (2004) analinganisha mazingira ya shule akisema yana athari kwa mitazamo ya wanafunzi wa lugha ya pili kwa ujumla.Anajadili ya kwamba iwapo wanafunzi hawatakamilisha shule wakiwa na upendo wa dhati katika ujifunzaji wao, watakosa kufaulu katika jamii-lugha ya leo. Earthman, (2004) anatazama nafasi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Anasema kwamba nafasi ni muhimu zaidi hata kuliko majengo. Anaeleza nafasi kama mwingiliano kati ya mazingira na nafasi ya jamii.

### 2.6.2 Mazingira na Nafasi Katika Ujifunzaji wa Lugha ya Pili

Earthman, (2004) anaainisha mifano ya mazingira na nafasi kama hali joto na hali ya hewa, jambo ambalo huweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili.Anataja pia kiwango cha juu cha kelele. Higgins na wengine (2004) wanaeleza kwamba kelele huathiri jinsi akili inavyofanya kazi. Kelele huathiri pia masomo na kukosa kukua vyema kiakili.Sundstrom (1987) anataja pia kipengee cha rangi. Anaeleza kuwa kwa kiwango kikubwa rangi huweza kuathiri ustadi na hamasa ya ujifunzaji wa lugha ya pili.

Kupitia kwa tafiti za awali, uchaguzi wa rangi huhusishwa na umri wa mwanafunzi. Rangi zilizokolea zaidi hufaa kwa wanafunzi wadogo ilhali rangi zisizokolea hufaa kwa vijana. Pia wavulana huvutiwa na mazingira yenye rangi ya kukolea ilhali wasichana huvutiwa na rangi ambazo hazijakolea sana. Higgins (2004) na wenzake wanasema kwamba kipengee hiki cha rangi ni kipengee ambacho kinatafitiwa zaidi na watafiti wengine wakiwa na mengi ya kuongezea. Culp (2006) anasema kwamba kutandaza picha za kuonekana huchangia pakubwa katika kuleta ufanisi.Anaelezea kwamba wanafunzi wana uwezo wa kutambua mifano halisi. Jambo ambalo laweza kuboresha umilisi wa lugha ya pili.

Msimamo wangu ni kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili huhitaji mazingira mazuri au nafasi inayofaa. Kwa mfano, wanafunzi wakiwa darasani huhitaji madirisha yaliyo na vioo ili wasiweze kuhisi unyiri na pia madarasa yao yawe na milango. Wanafunzi waweze pia kuwa na makabati ya kuhifadhi vitabu, ikiwa kuna raslimali ya kutosha wawe na maktaba. Mazingira yao yawe na miti na maua. Mambo haya yatawasaidia sana katika masomo yao. Wanafunzi hawa waweze kuwa na uwanja wa kuchezea hasa wakati wa mapumziko. Kwa upande mwingine, ingawa Higgins na wengine

(2005) wanasema kwamba matokeo ya wanafunzi huboreshwa zaidi iwapo wana mazingira ya kufaa, madarasa mazuri, mabwawa ya kuogelea, runinga na mengineo, lazima wanafunzi wao hao waweze kufanya bidii ili wafaulu katika ujifunzaji wa lugha.

## 2.7 Dhima ya Lugha Asili

Katika kujifunza lugha ya pili watoto hutambua lugha yao ya asili kwa kuiga mazungumzo ya watu wazima.Uwezo wao katika mawasiliano aidha hurekebishwa au kupongezwa. Baada ya kujifunza hivi, wao hukuza ujuzi wa ruwaza au tabia ambazo zinahusishwa na lugha hiyo. Hivyo basi huweza kuipokea lugha ya kwanza.

Lee, (1968) anasema kwamba ugumu na makosa mengi yanayopatikana katika lugha ya pili hutokana na athari za lugha ya kwanza. Jambo hili lina ithibati kwamba, katika ujifunzaji wa lugha ya pili, ikiwa maana ya neno katika muktadha fulani ni sawa katika lugha ya asili na vile vile katika lugha ya pili, matamshi yanaweza kuwa tofauti neno hilo linapotamkwa, kwa kuwa mwanafunzi atahamisha mbinu ya utambuzi kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili.

Ellis, (1985) anatoa mfano wa hali hii akisema kwamba, Mfaransa anapozungumza kwa Kiingereza, Kiingereza chake kitasikika kama kifaransa. Viwango vyake vya msamiati na sarufi vitaathiriwa pia na lugha ya asili. Aghalabu lugha ya asili huingia kati ya lugha ya pili na kusababisha athari katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Kwa hivyo, sifa za lugha ya asili hujidhihirisha katika lugha ya pili. Marton (1981) anasema kuwa tunapotazama lugha ya asili kisaikolojia, tunapata kwamba lugha hizi mbili hukosa kupatana kwa kiwango cha juu katika mifumo yao ya lugha ya lugha ya pili.

Kwa ujumla, tafiti zinaonyesha kwamba lugha ya kwanza ndio mhimili katika ujifunzaji kwa jumla. Kwa hivyo ni muhimu kwamba wanafunzi wote watumie lugha yao ya kwanza wanapoanza shule. Wanafunzi wanapojifunza kwa lugha yao ya kwanza wanakuwa na uwezo wa kuelewa lugha ilivyo kwa kina.

### 2.7.1 Sera ya Lugha

Hivi karibuni, Wizara ya Elimu nchini Kenya imekuwa na maelekezo kwamba wanafunzi chini ya umri wa miaka minane wapokee maelekezo kwa lugha ya asili kama sehemu ya marekebisho ya mtaala.

UNESCO (1953), pia ilipendekeza ya kwamba lugha ya asili itumiwe katika elimu. Walijitetea kwamba ili mtoto akuzwe kijamii na kiakili, anahitaji kwa kiasi kikubwa lugha yake ya asili. Kwa kupitia ushawishi wa wanajopo kuhusu sera ya lugha, mapendekezo ya lugha ya asili kufunzwa katika madarasa kuanzia 1 hadi ya 3 yalipitishwa. Kupitia pia kwa malengo ya kitaifa kuhusu elimu; lugha ya asili ilipendekezwa kutumiwa katika madarasa ya mwanzo Kenya.

## 2.8 Vipengele Visivyohusika na Lugha

Jambo la hakika kuhusu kujifunza kwa lugha ya pili ni kwamba wanafunzi fulani hufaulu kujifunza lugha ya pili kuliko wengine. Kuna vipengele ambavyo husababisha jambo hili kuzuka. Vipengele hivi ni vile ambavyo havihusishwi na lugha kwa mfano, umbali wa kijamii, tofauti za kiumri, tofauti za vipaji, motisha, mikakati katika ujifunzaji, kushawishiwa na marika, lugha inayotumiwa kanisani, viongozi, hadhi na ajira.Vipengele hivi tunavieleza hapa kimoja baada ya kingine.

### 2.8.1 Umbali wa Kijamii

Kuna nyakati mbalimbali ambapo mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili hahisi mvuto wowote na jamii-lugha lengwa. Wanafunzi hivyo basi hubuni umbali wa kisaikolojia na vile vile umbali wa kijamii baina yao na wazungumzaji wa jamii-lugha lengwa. Miingiliano yao basi hupungua.

Schumann (1978a, 1978b) analifungamanisha suala hili na ule anaouita mtindo wa uzoeaji wa kitamaduni. Anaueleza kama kiathiriwa kisababishi cha ujifunzaji wa lugha ya pili. Anasema ikiwa wazungumzaji watapata uzoeaji wa kitamaduni watajifunza lugha ya pili lakini wasipopata uzoeaji huu hawawezi kujifunza lugha ya pili. Umbali kama huu wa kijamii ndio husababisha kuwepo kwa lugha za Pijini, ambapo kikundi kimoja hutawala kikundi kingine.

Mtindo huu wa Schumann husisitiza uhusiano kati ya mwanafunzi anayejifunza lugha na jamii-lugha lengwa. Mtindo huu hutumia nadharia ya kuwa, mwanafunzi wa lugha ya pili anapopata uzoefu katika jamii-lugha lengwa, mwanafunzi huyo atakuwa stadi katika lugha lengwa. Mtindo wake Schumann unajadili viathiriwa vinane ambavyo huathiri ubora wa mawasiliano. Viathiriwa hivi ni vile ambavyo wanafunzi wa lugha ya pili wanao kuhusu lugha lengwa. Anataja viathiriwa hivyo kama; kutawaliwa kijamii ambapo pana aidha upinzani au kujifunza kwa lugha ya pili, usimulishaji, uhifadhi, na marekebisho. Kuzungukwa yaani kushirikiana katika majengo ya kijamii kama vile shule, hospitali na vilabu. Mshikamano mkubwa, ulinganifu, mitazamo na muda wa makazi huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Kwa mfano ikiwa mwanafunzi atakaa katika eneo moja kwa muda, basi atakuwa na msukumo wa kujifunza lugha lengwa.

Freeman na Long (1991) wanahakiki mawazo ya Schumann (1978) ambapo wanasema Schumann hakubainisha viwango vya kijamii ambavyo husababisha matokeo ya lugha. Kama wao, Baker (2001) anasema umbali huu hubadilika jinsi mwanafunzi wa lugha ya pili anavyoendelea kupokea lugha lengwa. Baker anaendelea kusema kuwa maono ya Schumann hayakuzingatia vipengele muhimu kama vile umri, kutengana kwa jamii na uzoefu kuhusu elimu ya awali. Anasema mambo haya yanachangia katika kuamua jinsi mwanafunzi anavyofaulu kujifunza lugha ya pili katika mazingira mapya.

Mwanafunzi ambaye ana uzoeaji wa kitamaduni huweza kupokea lugha iwapo ana nafasi ambayo inamwezesha kupokea lugha hiyo. Pia, ikiwa anafanya kila juhudi kujifunza lugha hiyo hata asipokuwa darasani, yaani mazingira yaliyo nje ya darasa lake, mwanafunzi huyu anahisi mvuto katika jamii-lugha lengwa.

### 2.8.2 Tofauti za Kiumri

Kuna chukulizi kuhusu ujifunzaji wa lugha ya pili ambapo inashikiliwa kwamba wanafunzi wachanga hujifunza lugha ya pili kwa urahisi zaidi kuliko wale wazima. Penfield na Roberts (1959) wanahoji kuwa, muda wa kupokea lugha huwa kati ya miaka kumi ya kwanza, katika maisha na kwamba wakati huu bongo lina uwezo zaidi wa uhifadhi.

Seliger, (1978) anapendekeza kwamba kuna vipindi viwili tofauti katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Kipindi cha umakinifu au kipindi nyeti. Brown (1985) anasema kwamba kuna haipothesia inayoeleza kuwa kibayalojia kuna kipindi ambacho lugha hupokelewa kwa urahisi na kipindi hicho kikipita, sio rahisi kuipokea lugha ya pili.

Wengi wa wanafunzi wa lugha ya pili, hawafikishi viwango vinavyohusu uwezo ulio sawa wa mzungumzaji wa lugha ya kwanza.Kwa mfano, Burstall, (1975) katika uchunguzi wake kule Uingereza na Wales analinganisha makundi mawili ambayo yana 'uzoefu wa miaka mitano'katika ujifunzaji lugha. Kikundi kimoja kilianza kujifunza Kifaransa kwenye umri wa miaka minane ilhali kikundi cha pili kilianza wakiwa na miaka kumi na moja katika shule ya Sekondari. Anasema wale wa miaka kumi na moja walikuwa na uwezo zaidi ya wenzao.Walipolinganishwa wakiwa na umri wa miaka kumi na sita, wale walianza kujifunza Kifaransa wakiwa shule ya upili walifanya vyema kuliko wenzao. Mitihani yao ilihusu kuzungumza, kusoma na kuandika, walishindwa tu katika mbinu ya usikilizaji. Singleton, (1989) anahitimisha kwa kusema ya kuwa wale wanaojifunza lugha ya pili wakiwa wachanga wanapata ustadi zaidi kuliko wale wanaoanza wakiwa vijana au watu wazima.

Lenneberg (1967), anataja vipengele vinne ambavyo vinatoa maelezo kuhusu ubongo wa mtoto ukilinganishwa na ule wa mtu mzima. Anataja sababu za kibayolojia, sababu zinazohusu akili, zinazohusu hisia na zile zinazohusu mazingira ya watoto na watu wazima. Kwa hali hii basi, ubongo wa mtoto na ule wa mtu mzima hutofautiana ambapo chanzo chake ni mtafaruku wa kiumri.

### 2.8.3 Tofauti za Vipaji

Caroll (1987) anaeleza vipaji kama uwezo ambao wanafunzi wa lugha wanao. Hatambui kufaulu au kutofaulu kwa mwanafunzi ila hudhihirisha sababu zinazochangia wananafunzi fulani kujifunza lugha kwa haraka kushinda wenzao.

Skehan, (1989) anasema vipaji ni vipengele vikuu katika utabiri wa ufanisi katika kujifunza lugha ya pili. Ellis, (1997) anasema ingawa watu binafsi hawaonyeshi tofauti zozote katika lugha ya asili, tofauti hizi hudhihirika wazi katika lugha ya pili

hasa tunapoviangalia vipengele kama vile kiasi, kasi na viwango vya ujifunzaji wa lugha ya pili. Kuna vipengee vinavyohusu akili, hisia na vinavyohusishwa na jamii.

Vipaji vina manufaa hasa kwa elimu kwa sababu huweza kutambua uwezo na udhaifu wa mwanafunzi kwa hivyo tunapozingatia hiki kipengee cha vipaji, mwalimu wa lugha ya pili huweza kufaidika kwa kuwaelewa wanafunzi wake vyema.

Gardner, (1985) anapendekeza motisha huku Schumann, (1978) akipendekeza uzoeaji wa utamaduni utumike katika uhakiki wa vipaji. Neufeld (1978) anapendekeza nafasi ilhali Heberd, (1975) naye anapendekeza mitazamo kuwa ina umuhimu zaidi kwa ujifunzaji wa lugha ya pili kuliko vipaji.Herberd anasema hivi kwa msingi kwamba, ukadiriaji wa vipaji aghalabu haujahusishwa katika tafiti nyingi. Kwa mfano, katika maono ya Schumann, (1978) hajazingatia mambo ya vipaji. Kuna uhakiki kwamba kipengee cha vipaji ni cha asili. Wesche, (1981) anasema lazima tuelewe vipengee vinavyosababisha mambo haya. Hii ni kwa sababu kuna wanafunzi tofauti tofauti.Krashen (1981, 1985) anasema vipaji hufaa tu kwa ujifunzaji lugha darasani. Anasema vilevile kwamba, kuna vipengee vitatu katika vipaji; kumbukumbu, uwezo wa kuchanganua lugha na uwezo wa kupanga kanuni kifonimu. Krashen anasema kuwa uwezo wa kuchanganua lugha huweza kutumiwa tu katika muktadha wa darasa.

### 2.8.4 Motisha

Corder (1973) anasema kwamba tukiwa na kipengee hiki cha motisha, kila mmoja wetu ana uwezo wa kujifunza lugha ya pili. Motisha huweza kupatikana katika muktadha wa kujifunza lugha hasa darasani. Pia huweza kupatikana baada ya ufanisi wa wanafunzi hasa wanapopokea zawadi. Motisha huweza kuathiriwa na vipengee kama vile walimu stadi, mitihani na hata zawadi.

Wanadharia ambao wanatambulika sana katika uwanja huu ni Robert Gardner na Wallace Lambert wakichangia mawazo ya Mowrer (1950) aliyesisitiza umuhimu wa kujitambulisha na mtu aliye na thamani. Gardner na Lambert (1959, 1972) walichangia mawazo yake na kusema kuwa watu huchangamkia kujitambulisha sio tu na watu wenye thamani, bali pia wageni kutoka nje. Jambo hili ndilo lilizua mitazamo mbalimbali kwa kuathiriwa na wazazi mazingiria ya nyumbani, na tamaduni asili. Gardner na Lambert walisema kwamba wanojitambulisha na wageni kutoka nje hufanya hivyo ili kuelewa tamaduni zao, na kujishirikisha na tamaduni zenyewe. Jambo hili hasa inahusishwa na nafsi ya mwanafunzi. Wanasema utambulishokama huu huweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili na kuleta mafanikio.

Gardner na Lambert, (1972) wanazungumza wakihusisha maelekezo ya mazingira kuhusu kujifunza lugha ya pili. Motisha hii iliangazia manufaa ambayo hupatikana mzungumzaji anapokuwa na ujuzi wa lugha ya pili. Walitoa mifano kama weledi, uwezo wa kufanya kazi vyema, uwezo wa kusoma kazi katika lugha lengwa na uwezo wa kutangamana na tamaduni ngeni. Gardner (1985) alibuni kisawazishi kuhusu motisha kwamba; motisha= jitihada +hamu ya kujifikia lengo + mitazamo. Anataja vipengee katika jitihada hizi kama vile hamu ya kumfurahisha mwalimu, ama mzazi, tarajio kuu la kufikia malengo na tabia nzuri za masomo. Gardner anahusisha mitazamo na tabia ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Hapa ndipo tunapopata ujifunzaji wa lugha ya pili. Walimu wengi pamoja na watafiti wanakubaliana ya kwamba motisha ina umuhimu katika kuamua kufaulu au kutofaulu katika muktadha wowote wa kujifunza lugha ya pili.

Skehan, (1989) anaeleza kwamba kuna aina mbili za mielekeo kuhusu motisha.Motisha inayohusisha na motisha inayounganisha. Tunapoangazia motisha inayounganisha tunapata kwamba, mwanafunzi ana haja ya kujifunza lugha ya pili ili kuwasiliana na wazungumzaji wa jamii-lugha lengwa. Motisha inayohusishwa kwa upande mwingine ni motisha ambayo mwanafunzi hana haja na jamii- lugha legwa ila anahaja au hitaji la kujifunza lugha lengwa ili ajifaidishe yeye binafsi labda kimasomo ama kikazi.

Inavyoelekea basi ni kwamba, ni muhimu kwa walimu kuwaelewa wanafunzi wao wa lugha ya pili. Ni muhimu walimu waweze kuelewa usuli na mitazamo ya wanafunzi wanaowafunza lugha ya pili. Wakati mwingine mazingira ya wanafunzi si mazingira yaliyo na motisha ya kujifunza lugha ya pili. Kama mwalimu, panga ili wanafunzi wajihusishe na michezo inayowapa motisha ya lugha baada ya masomo. Wanafunzi wanafaa kuzuru hata maeneo tofauti tofauti. Mwalimu anayejifunza lugha ya pili afanye mipangilio ili wazungumzaji maalum kutoka nje ya shule waweze kuwatembelea ili kuwachangamsha kuhusu kazi za usoni. Wanafunzi waweze kununuliwa magazeti na mara moja moja wazitazame filamu zinazohusu lugha ya pili za kuwafaa kama vile "Black Board Jungle,"na "The Breakfast Club," pamoja na"Stand by Me," ambazo huweza kuwafaa wanafunzi wa Kiingereza kama lugha ya pili.

### 2.8.5 Mikakati katika Ujifunzaji wa Lugha

Cohen, (1998) anaelezea mikakati katika ujifunzaji wa lugha ya pili kama michakato ambayo huchaguliwa na wanafunzi na ambayo hunufaisha ujifunzaji wa lugha ya pili. Kuna aina tatu za mikakati kwa mujibu wa Ellis (1994). Anataja uzalishaji, mawasiliano na kujifunza, Tarone, (1980b) anaeleza mikakati katika kujifunza lugha

ya pili kama uwezo wa kukuza umilisi kiisimu na kiisimu jamii, katika lugha lengwa. Umilisi kiisimu jamii huzingatia wanafunzi kuwa na mbinu za kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika.

Mbinu ambazo hutumiwa katika kutafiti mikakati katika lugha ya pili ni kama vile, kuwachunguza wanafunzi wakifanya kazi tofauti tofauti hasa katika miktadha ya darasa. Rubin, (1981) anahakiki mbinu hii kwa kusema kwamba kuchunguza tu hakuwezi kukadiria mambo ya akili na kuwa darasa lina nafasi finyu inayomwezesha mtafiti kuchunguza mikakati katika lugha. Chesterfield na wengine, (1981) wanasema kuwa uchunguzi una manufaa tu kwa watoto wadogo lakini si kwa watu wazima.

Naiman na wenzake, (1978) Rubin (1981), Politzer na wenzake, (1985) na Oxford (1985) wanasema kuwa mikakati inayofaa zaidi ni matumizi ya mahojiano na hojaji. Mikakati kuhusu matumuzi ya shajara ambazo hueleza maoni kuhusu hisia inapendekezwa na Brown (1985).

Vipengee vinavyoathiri uteuzi wa mikakati ni kama vile; mitazamo, vipengee vinavyohusu hisia na vipengee vingine kwa jumla. Kuna kipengee cha umri ambacho pia huathiri kujifunza kwa lugha ya pili. Oxford na wenzake. (1989) wanataja kipengee kingine ambacho ni motisha. Earthman, (1990) analinganisha usuli wa mwanafunzi na mikakati katika kujifunza lugha ya pili. Politzer, (1983) anataja vipengee kama lugha inayofunzwa, muktadha wa ujifunzaji, kazi ambazo mwanafunzi anafanya, jinsia, na nafsi kama vipengele vinavyoathiri uteuzi wa mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili.

Katika kufafanua uhusiano baina ya mikakati ya lugha ya pili na ukuzaji wa lugha ya pili, wanafunzi waliofaulu hutumia mikakati ya lugha zaidi kuliko wanafunzi ambao hawajafaulu. Wanafunzi stadi wana uwezo wa kuwa makini zaidi ya kujifunza lugha ya pili. Mikakati mbalimbali hukuza umilisi wao katika lugha ya pili.

Mikakati kuhusu lugha hubainisha tofauti ambazo hupatikana baina ya wanafunzi. Tafiti nyingi zimeainisha mikakati inayofaa kutumiwa lakini ni jambo ambalo lazua mijadala kwa sababu mikakati inayotumiwa hujiegemeza kwenye malengo yake.

### 2.8.6 Kushawishika na Marika

Vijana kwa kiasi kikubwa huathiriwa na marika zao katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ushawishi kutoka kwa marika kwa kiasi kikubwa huekua malengo ya wazazi na walimu. Wao hubuni tabia tofauti tofauti, ruwaza au mitazamo ili kujitambulisha na kundi fulani. Jambo hili huwa na mshiko kwani katika kipindi hiki, vijana hutafuta utambuzi kutoka kwa marafiki zao na kujitenga na wazazi.

Ushawishi huu huweza kutoka kwa marafiki, wenzi shuleni, na athari ambazo zinatokana na miziki, runinga na mtandao.Walqui (2000) anaeleza ya kwamba ushawishi wa marika huathiri ufanisi katika kujifunza lugha ya pili na huzua mitazamo hasi.

### 2.8.7 Lugha inayotumika Kanisani

Lugha inayotumiwa kanisani huweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Viongozi kanisani na waumini wanapaswa kutumia lugha ya pili katika maombi yao, katika mahubiri yao, katika nyimbo na hata wakati waumini wanatoa ushuhuda kanisani. Wakalimani waweze kutumia lugha sanifu.

### 2.8.8 Viongozi

Viongozi wana jukumu la kuendeleza ujifunzaji wa lugha ya pili. Wanapaswa kuwa vielelezo kwa ujifunzaji wa lugha ya pili.Kwa mfano, wabunge wanapopitisha miswada bungeni, wanapaswa kutumia lugha ya pili iliyo sanifu na kwa kufanya hivi huweza kuigwa na umma wa wasikilizaji wao.

### 2.8.9 Hadhi

Tunapozingatia mambo kuhusu rejesta na lahaja ya lugha pamoja na uhusiano baina ya lugha mbili tofauti; hadhi yazo hujumuishwa pamoja na tamaduni. Wanafunzi ambao lugha yao ya asili ina hadhi ya chini kuliko lugha yao ya pili, hupoteza lugha yao ya kwanza; na vilevile tamaduni zinazohusiana na lugha hiyo ya kwanza. Wao hujiunga na lugha ya pili ambayo huonekana kuwa na hadhi ya juu kuliko lugha asilia.

### 2.8.10 Ajira

Wakati fulani lugha ya pili inapokosa kuwa na hadhi, wanafunzi wengi huwa na kasumba kwayo. Wengi wa wazungumzaji wa lugha ya pili huwa na umilisi katika lugha ya asili na kukosa umilisi katika lugha ya pili, jambo ambalo huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili.

## 2.9 Mitazamo ya Wanafunzi

Jambo la mitazamo limeshughulikiwa na wananadharia wengi wa lugha. Ujifunzaji wa lugha ya pili huathiriwa na mitazamo na motisha ya wanafunzi. Wanafunzi ambao wana motisha na wale wasio na motisha wana mielekeo tofauti tofauti kuhusu walimu wao na mtaala. Mielekeo yao huathiri mitazamo yao. Meenakshi, (2008) anasema kuwa mtu binafsi ana mielekeo tofauti kuhusu mwalimu wake, rika lake, mtaala na mahitaji yake ambayo huathiri mitazamo yake kuhusu lugha ya pili. Ikiwa wanafunzi

wanamtazama mwalimu wao kama aliye na tabia nzuri na anayetekeleza wajibu wake vizuri, watampenda na kuwa na mitazamo chanya kuhusu lugha ya pili anayoifundisha. Wanafunzi wanahitaji mwalimu ambaye atawapa motisha ya kuzungumza zaidi wakiwa darasani na anayeweza kuwafunza kuhusu jinsi ya kutumia lugha wakiwa darasani. Wanafunzi wanahitaji mwalimu ambaye ana lugha sanifu na anayeweza kurekebisha makosa yao vilivyo.

## 2.10 Mitazamo ya Walimu

Mitazamo ya walimu huchangia kwa kiasi kikubwa katika kujifunza lugha ya pili. Hapa ni pale ambapo walimu wameacha kuwa waelekezi na kuwa wasaidizi wa wanafunzi. Wanatekeleza majukumu ya kuwarekebisha wanafunzi wao makosa yao na kuwapa motisha katika kutumia lugha husika kwa wingikatika maisha yao ya kila siku. Tabia yake mwalimu kwa wanafunzi wake huathiri kwa kiasi kikubwa mitazamo ya wanafunzi kuhusu lugha.

Savington, (1991) akizungumzia umuhimu wa mitazamo anahoji kuwa katika kuboresha ujifunzaji, mwalimu wa lugha amenyimwa nafasi yake. Richards na wenzake (1994) wanasema kuwa majukumu yote ambayo yanatekelezwa na walimu ni yale wanayoyaelewa. Ujuzi wake mwalimu ndio ambao humsaidia katika kutekeleza wajibu wake akiwa darasani.

## 2.11 Mitazamo ya Wazazi

Wazazi pia wana jukumu la kutekeleza katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ikiwa watakuwa na mitazamo hasi kuhusu lugha ya pili, bila shaka hata watoto wao watakuwa na mitazamo hasi. Ni wajibu wa wazazi kuwaelekeza watoto wanaporudi nyumbani kutoka shuleni. Hii ina maana kuwa wazazi waweze kuzungumza lugha hiyo ya pili na kuonyesha hitaji kuu la lugha husika. Katika mawasiliano kwa kutumia

lugha hiyo ya pili, ikiwa wana uwezo, wawape wale watoto mahitaji yote ambayo yanahitaji ujifunzaji wa lugha hiyo. Watoto wanapopewa mazoezi ya ziada, wazazi wawe katika mstari wa mbele kuhakikisha kuwa kazi hiyo imefanywa vyema.

Iwapo wana uwezo, wanaweza kuwahimiza kutazama runinga na kusikiliza redio ili waweze kuboresha matumizi yao ya lugha hiyo ya pili. Ikiwa watoto wao wamefanya makosa katika mazungumzo yao, wazazi waweze kuwarekebisha bila kuwaaibisha. Yaani wazazi wawe vielelezo kwa ujifunzaji lugha ya pili kwa wana wao hasa wakiwa manyumbani.

### 2.12 Hitimisho

Kutokana na sura hii, imebaini kwamba, mwingiliano ni muhimu kwani hukuza ujifunzaji wa lugha.Tumepata pia kwamba, kuna viathiriwa vinavyoathiri wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Viathiriwa hivi vikiwa pamoja na, vipengee tambuzi, vipengee vinavyohusiana na hisi za watu katika ujifunzaji wa lugha ya pili, vipengee vinavyohusu akili, vipaji, nafsi, motisha, mitazamo, mapendeleo na imani ya wanafunzi na umri wao katika kujifunza lugha ya pili. Tumejadili pia vipengee visivyohusika na lugha katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Vipengee tulivyovitaja ni pamoja na umbali wa kijamii katika kujifunza lugha ya pili, tofauti za kiumri,tofauti za vipaji, motisha, mikakati katika ujifunzaji wa lugha ya pili, kushawishiwa na marika, lugha inayotumiwa kanisani, viongozi kama vielelezo katika ujifunzaji wa lugha ya pili na kipengee cha ajira katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Pia tumejadili kwamba, ili mitazamo ya wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili iwe chanya, ni lazima mitazamo ya wazazi na walimu katika ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya pili iwe chanya.

# SURA YA TATU

# VIPENGEE VINAVYOATHIRI MITAZAMO YA WAZUNGUMZAJI WA KIJALUO KWA LUGHA YA KISWAHILI

## 3.1 Utangulizi

Utafiti uliofanywa ni kifani cha jimbo dogo la Marindi iliyo katika Kaunti ya Migori. Sampuli kielelezo ni shule nne za msingi katika eneo hilo la Marindi; zikiwa shule za Assar Johansson, Ragana, Migori pamoja na Nyanko. Utafiti ulihusu madarasa mawili; la sita na vile vile la saba. Madarasa haya yaliteuliwa kwa sababu wanafunzi wayo, wana uwezo wa kujieleza vyema wakilinganishwa na wale wengine wa madarasa ya chini. Darasa la nane halikuteuliwa kwa sababu wanafunzi wake wanashughulika na maandalizi ya mitihani yao ya kitaifa. Sura hii inawasilisha na vilevile kuchanganua data tuliyopata katika kushughulikia mada yetu ya utafiti.

## 3.2 Watafitiwa katika Utafiti

Jumla ya wanafunzi ishirini na wanne walihojiwa kwa kutumia hojaji ambazo zilisambazwa katika kila shule. Wanafunzi sita walipewa hojaji za kujazwa. Baadaye, kulikuwa na majadiliano katika makundi. Nilitaka wanafunzi wale waelezee, kupitia kwa majadiliano vipengee vingine kama vile motisha, kushawishiwa na marika, lugha inayotumika kanisani na viongozi.

Walimu wawili kutoka katika kila shule walipewa hojaji ili waweze kuzijaza. Kwa ujumla walimu walikuwa wanane. Walimu waliopewa hojaji walikuwa mmoja mmoja katika darasa la sita na mmoja katika darasa la saba katika kila shule. Mwalimu husika alipaswa kuwa mwalimu wao wa Kiswahili. Niliwahusisha walimu wakuu wa shule hizo katika majadiliano ya ana kwa ana kuhusiana na mada yetu ya utafiti. Kwa ujumla, walikuwa walimu wakuu wanne.

Wazazi waliozipokea hojaji kwa ajili ya kuzijaza walikuwa kumi na wanne. Umri wa waliohojiwa ulikuwa kati ya miaka 18 hadi 35. Sababu ya kuchagua wahojiwa wa umri huu ni kwamba, ni watu wazima ambao wana uwezo wa kutoa habari kamili kuhusu fikra au hata mitazamo yao kuhusu lugha hii ya Kiswahili.

Kwa jumla sampuli kielezo ilihusu watu hamsini. Sampuli iliyotumiwa ilikuwa sampuli ya kusudi. Viathiriwa kwa ajili ya utafiti huu, vilihusu umri, jinsia, makazi na viwango vya elimu. Wale wanafunzi waliozipokea hojaji za kujaza walijumuisha wanafunzi ishirini na wanne. Wanne hawakuzijaza nafasi zote katika hojaji kwa hivyo walioshughulika walikuwa wanafunzi ishirini tu. Vilevile, wazazi sita hawakukamilisha kujaza hojaji zao. Kwa hivyo, walisalia watu arubaine tu. Sikuweza kushughulikia majibu ya kila mhojiwa bali niliangalia mawazo yaliyosawa kisha nikayachanganua kwa kutumia nambari pamoja na asilimia.

**Jedwali 3.1: Jumla ya Walengwa katika Utafiti na Jinsia Zao**

| Walengwa | Kike | Kiume | Kike % | Kiume% |
|---|---|---|---|---|
| Walimu wakuu | 0 | 4 | 0 | 100 |
| Walimu wa Kiswahili | 6 | 2 | 75 | 25 |
| Wanafunzi wa darasa la 6 | 7 | 3 | 70 | 30 |
| Wanafunzi wa darasa la 7 | 6 | 4 | 60 | 40 |
| Wazazi | 5 | 3 | 62.50 | 37.50 |
| Jumla | 24 | 16 | | |

Hapo awali wazazi waliolengwa walikuwa wa kike 7 na kiume 7. Wanafunzi waliozijaza hojaji walikuwa wa kike 3 na wa kiume 3 katika kila shule. Utafiti ulionyesha ya kwamba walimu wakuu katika shule hizi nne zinazopatikana katika

jimbo la Marindi wote walikuwa wa kiume ndiposa tunasema ni asilimia 100. Vilevile katika walimu wanane wa Kiswahili, wawili tu ndio waliokuwa wa kiume ilhali sita walikuwa wa kike. Yaani, asilimia 25 na 75 inawakilisha walimu wa Kiswahili walio wa kike na kiume mtawalia. Walengwa kutoka katika darasa la sita waliozijaza hojaji na kukamilisha walikuwa wavulana 3 na wasichana 7 ambao ni wa kike na kiume, asilimia 30 na 70 mtawalia. Hali katika darasa la 7 ilikuwa asilimia 40 na 60 mtawalia. Wazazi waliojaza hojaji walikuwa wa kike asilimia 62.5 na wa kiume asilimia 37.5.

### 3.2.1 Vipengee Visivyohusika na LughaVinavyoathiri Mitazamo Visivyo vya Kilugha

Vipengee vilivyotafitiwa ni pamoja na; umbali wa kijamii, tofauti ya kiumri, tofauti za vipaji, motisha, elimu, kushawishiwa na marika, lugha inayotumika kanisani, viongozi, hadhi na ajira.

### 3.2.2 Umbali wa Kijamii

Umbali wa kijamii aghalabu husababishwa na ile hali ya mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili kutohisi mvuto wowote na jamii-lugha lengwa. Hivyo basi, watu hubuni umbali wa kisaikolojia na vile vile umbali wa kijamii baina yao na wazungumzaji wa jamii-lugha lengwa. Maingiliano ya watu walio na hali ya umbali wa kijamii hupungua (Schemann, 1978).

Kwa kutumia uelekevu wa kutambua pamoja na mahojiano, ilitambulika wazi kwamba katika eneo hili la Marindi kulikuwa na umbali wa kijamii kuhusu lugha hii ya Kiswahili. Jambo hili la umbali wa kijamii kuhusu Kiswahili lilisababisha mitazamo hasi miongoni mwa wazungumzaji wa Kijaluo. Vilevile kutoka kwa hojaji

40 zilizotolewa kwa ajili ya utafiti, walengwa 15 tu ndiowalionyesha shauku katika lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 3.2: Majibu Kutokana na Kipengee cha Umbali wa Kijamii**

| Jumla | Nambari chanya | % Chanya | Nambari hasi | % Hasi |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 16 | 40 | 24 | 60 |

Kutokana na jedwali hili, walengwa wote waliohojiwa walikuwa 40. Kwa kuzingatia kipengee hiki cha umbali wa kijamii, walengwa 16 walikuwa na mitazamo chanya kutokana na majibu yao ambayo ni asilimia 40 ya walengwa wote, ilhali kutokana na majibu ya walengwa, walengwa 24 walionyesha mitazamo hasi. Yaani, asilimia 60. Kwa ujumla kuna umbali wa kijamii katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Hii inadhihirisha kwamba, wengi wa watafitiwa hawahisi mvuto wowote kuhusiana na lugha ya Kiswahili. Maingiliano yao hivyo basi yamepungua.

**Jedwali la 3.3: Majibu Kutokana na Kipengee cha Umbali wa Kijamii kwa Kuegemea kwa Walengwa**

| Walengwa | Jumla | Nambari chanya | % chanya | Nambari hasi | % hasi |
|---|---|---|---|---|---|
| Walimu wakuu | 4 | 0 | 0 | 4 | 100 |
| Walimu wa Kiswahili | 8 | 8 | 100 | 0 | 0 |
| Wanafunzi wa darasa la 6 | 10 | 3 | 30 | 7 | 70 |
| Wanafunzi wa darasa la 7 | 10 | 4 | 40 | 6 | 60 |
| Wazazi | 8 | 1 | 12.5 | 7 | 87.5 |

Uwasilishaji huu unaonyesha bayana kwamba, kati ya walengwa 40, walimu wakuu wote walionyesha mitazamo hasi, walimu wote wa Kiswahili wakaonyesha mitazamo chanya na mzazi mmoja pekee ndiye aliyeonyesha mtazamo chanya. Miongoni mwa wanafunzi kutoka kwa darasa la sita ni watatu tu ndio walioonyesha mitazamo chanya ilhali katika darasa la saba walikuwa wanafunzi wanne. Majibu yameonyeshwa kupitia kwa asilimia kwenye jedwali.

### 3.2.3 Tofauti za Kiumri

Kuna haipothesia inayoelezwa kuwa kibayolojia kuna kipindi ambacho lugha hupokelewa kwa urahisi na kipindi hicho kikipita sio rahisi kuipokea lugha (Brown, 1985).

Kupitia kwa mahojiano ya makundi na wanafunzi, wengi wao walionyesha ustadi mwingi katika matumizi yao ya Kiswahili hasa kwa kuzingatia matamshi na lugha ya Sheng'. Kwa upande mwingine walimu wakuu walionyesha hali ya juu ya umilisi wa Kiswahili lakini sio katika utendaji hasa katika maandishi. Wengi wa walimu wale waliathiriwa na lugha ya mama na kushindwa kuielewa misamiati mingi katika hojaji hadi wakati ambapo niliitafsiri kwao. Walimu wa Kiswahili walionyesha umilisi na vilevile utendaji ulio sawa katika Kiswahili. Wengi wa wazazi hawakuwa na umilisi wa Kiswahili na vile vile waliathiriwa kwa kiasi kikubwa katika utendaji wao na lugha ya Kijaluo. Kuna wale waliojaribu kujieleza kwa ufasaha katika Kiswahili japo kwa kiasi kidogo.

**Jedwali la 3.4:Majibu Kutokana na Kipengee cha Tofauti za Kiumri**

| Jumla | Nambari chanya | % Chanya | Nambari hasi | % hasi |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 24 | 60 | 16 | 40 |

Kutokana na jedwali hili ni bayana kuwa mitazamo ya watafitiwa kuhusiana na lugha ya Kiswahili ni chanya. Kupitia kwenye mahojiano na majibu za hojaji, asilimia kubwa ya watafitiwa wenye umri mdogo kama vile wanafunzi wana mitazamo chanya kuliko watu wazima.

### 3.2.4 Tofauti za Vipaji

Kipaji ni uwezo wa kuzaliwa ambao humwezesha mtu kufanya jambo fulani.Vipaji kuhusu lugha hufaa katika ujifunzaji wa lugha. Kuna vipengee vitatu katika vipaji ambavyo ni kumbukumbu, uwezo wa kuchanganua lugha na uwezo wa kupanga kanuni kifonimu (Caroll, 1985 na Krashen, 1985.

Kwa kweli, watu walio na motisha huwa na vipaji vya juu katika ujifunzaji wa lugha. Wale walio na vipaji vya chini huwa na makosa mengi katika kujifunza lugha, makosa labda ya kisarufi. Kwa hivyo, utendaji wao ni wa chini ingawa Ellis (1994) akimnukuu Caroll (1987), anatuonya tusichanganye vipaji na utendaji.

Katika utafiti huu niligawa walengwa kuwili; kwa upande mmoja niliangalia wanafunzi na kwa upande mwingine watu wazima. Utafiti ulionyesha kwamba wanafunzi walikuwa na uwezo zaidi kuliko watu wazima, ingawa walikuwa na changamoto mbalimbali katika utumiaji wao wa Kiswahili. Changamoto zenyewe zilidhihirika wazi katika majibu yao ya maswali ya 15 na 16 katika hojaji.

15) Una shida zipi kama mwanafunzi katika kujifunza lugha hii ya Kiswahili?

16) Mawazo yako ni yapi katika kuinua viwango vya somo la Kiswahili katika shule yenu?

Watu wazima kwa upande mmoja walionyesha vipaji vya chini wakilinganishwa na vipaji vya wanafunzi. Hili ni jambo ambalo lilidhihirika wazi katika utendaji wao. Wengi wa wazazi waling'ang'ana na lugha ya Kiswahili wakati wa kujibu maswali. Walionekana kuathiriwa na lugha ya mama na vilevile kuonekana kukosa motisha. Wengi walisema lugha ya Kiswahili si lugha yao na kwamba si lazima waitumie katika mawasiliano.

**Jedwali la 3.5: Majibu kwa Kuegemea Umri**

| | **Chanya** | **% Chanya** | **Hasi** | **% hasi** |
|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi 20 | 15 | 75 | 5 | 25 |
| Watu wazima 20 | 8 | 40 | 12 | 60 |
| Jumla | 23 | 57.50 | 17 | 42.50 |

Asilimia 57.50 ilitetea kauli kwamba kipengee cha vipaji ni muhimu katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

### 3.2.5 Motisha

Motisha kwa kiwango kikubwa husaidia katika kuleta ufanisi katika kujifunza lugha ya pili kama vile Kiswahili katika jimbo dogo la Marindi.

Kwa kuzingatia swali ya 17 katika hojaji, ni wanafunzi wawili tu katika shule moja ndio walijibu kwamba hawazawadiwi wanapofanya vizuri katika mtihani.Wengine wote walikiri kuwa wao huzawadiwa. Swali lilikuwa,

17) Wanafunzi wote ambao wamefanya vizuri katika mtihani hupewa zawadi.?

Ingawa wanafunzi wanapofanya vizuri wanazawadiwa, walimu ni kikwazo kikubwa katika ujifunzaji wa lugha hii. Hii ni kutokana na majibu kuhusu changamoto wanazokumbana nazo. Kwa mfano kuwa, katika kufunza somo la Kiswahili, wengi wa walimu hawana uelewa wa kutosha wa lugha hii ya Kiswahili. Pia walimu hawapeani mazoezi ya kutosha na wengine wao hata hukosa kusahihisha kazi zenyewe.

Walimu walionyesha hali ya kukosa motisha hasa walipotaja ya kwamba hawapati vifaa vingi vya kufunzia. Wengi katika kulijibu swali la 20; walikiri kwamba kipengee cha motisha ni jambo muhimu katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili Marindi. Vile vile wazazi wote walikiri ya kwamba swala hili la motisha ni muhimu sana katika kuamua kufaulu au kutofaulu katika muktadha wowote wa kujifunzia lugha ya Kiswahili Marindi. (maswali ya viwango, swali la 20). Katika majadiliano ya kipengee cha hojaji nambari 18, walimu wakuu walikiri kwamba motisha ni muhimu.Hata hivyo, walikosa kuyatimiza malengo ya wanafunzi wao na vile vile walimu, kwa kutowapa vifaa vinavyohitajika katika kujifunza na kuifunza lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 3.6: Majibu Kutokana na Kipengee cha Motisha**

| Jumla | Nambari chanya | % chanya | Nambari hasi | % hasi |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 35 | 87.50 | 5 | 12.5 |

Kutokana na jedwali hili, kipengee cha motisha ni kipengee muhimu katika kujifunza na kufunza lugha ya Kiswahili.

### 3.2.6 Elimu

Kiswahili kimepewa umuhimu mkubwa katika elimu nchini mwetu. Kiswahili ni lugha ya taifa inayowakilisha jamii yenye watu wenye makabila tofauti kisiasa, kijamii na kitamaduni (Mathooko, 2007).

Katika jimbo dogo la Marindi, lugha hii ya taifa inasusiwa na wengi, na kupitia kwa utafiti uliofanywa, wengi wa wakazi wa eneo hili wana mitazamo hasi kukihusu Kiswahili. Kupitia kwa uelekevu wa kutambua hasa katika miktadha ya shule, na ya kanisa, lugha inayotumiwa sana ni lugha ya asili ya Kijaluo. Walimu wanapokuwa katika chumba chao, hutumia lugha ya asili na hata mawasiliano baina yao na wanafunzi huwa katika Kijaluo. Hata wale walimu wa Kiswahili katika Marindi hawajaachwa nyuma.Kwa hivyo, lugha inayotumiwa sana ni lugha ya asili ya Kijaluo na Kiingereza. Wazazi pia hawajawa vielelezo kwa utumiaji wa Kiswahili hasa kwa watoto wao. Kwa hivyo,wazazi wana mchango mkubwa katika kusababisha vikwazo katika lugha hii ya Kiswahili.

**Jedwali la 3.7: Majibu Kutokana na Kipengee cha Elimu**

| Jumla | Nambari chanya | % chanya | Nambari hasi | % hasi |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 15 | 37.5 | 25 | 62.5 |

Kutokana na jedwali hili asilimia 62.5 ya watafitiwa wana mitazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, wengi wa watafitiwa hawaitumii sana lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao na hata katika asasi mbalimbali ziwe rasmi au za jamii. Jambo linalosababisha mitazamo hasi miongoni mwao.

### 3.2.7 Kushawishiwa na Marika

Kwa mujibu wa Earthman, (2004) Ubora wa mazingira ya wanafunzi huathiri uwezo wao na jinsi wanavyojifunza. Mazingira haya yanaweza kuhusu mwanafunzi, au hata wanafunzi wengine. Mazingira huwabadilisha wanafunzi kitabia na vile vile kuwaathiri.

Kutokana na utafiti wetu, wengi wa walengwa wameathiriwa sana kwa mujibu wa swali la 3 ambalo liliuliza vifuatavyo:

3) Lugha unayoienzi kabisa ni ipi?

Kiswahili ☐ Kiingereza ☐ Sheng' ☐

Wengi walichagua Sheng' na Kiingereza. Ndiposa katika utafiti huu walimu wakuu walikiri aidha kuzitumia lugha ya Kiingereza au lugha ya asili. Vile vile walimu wengine walikiri kuitumia lugha ya asili ya Kijaluo katika miktadha ya shule. Jambo linaloonyesha ya kwamba wameathiriwa na lugha ya mazingira yao.

**Jedwali la 3.8: Majibu Kutokana na Kipengee cha Kushawishiwa na Marika**

| Jumla | Nambari chanya | % chanya | Nambari hasi | % hasi |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 25 | 62.50 | 15 | 37.50 |

Kwa hivyo, kipengee hiki kimeathiri mitazamo ya wakazi wa eneo la Marindi dhidi ya lugha ya Kiswahili.

### 3.2.8 Lugha Inayotumika Kanisani

Katika kushughulikia kipengee hiki, nilitumia kinasa sauti kanisani ili kubaini matumizi ya lugha ya Kiswahili ambayo ilikuwa duni. Kutokana na maswali ya viwango swali la 9 na ambalo lilisoma vifuatavyo:

9) Lugha ya Kiswahili hutumiwa katika jimbo hili kuendeleza mahubiri?

1 2 3 4 5

Tia mviringo (0) kuonyesha kuwa;

1. Ninakubaliana kabisa.
2. Ninakubaliana.
3. Sikubaliani kabisa.
4. Sikubaliani.
5. Sina maoni.

Katika majibu yao, wengi walisema, aidha hawakubaliani au hawakubaliani kabisa. Kupitia kwa majadiliano baina yangu na wanafunzi, walimu na wazazi, wengi walisema lugha ya Kiswahili haitumiwi katika kuendeleza mahubiri, matangazo, sala na nyimbo makanisani. Walimu wakuu katika majibu yao kwa nambari 19 na ambapo swali liliuliza vifuatavyo:

19) Lugha gani hutumiwa katika kanisa lenu? Unaweza kusema lugha hii ina athari yoyote kwa wanafunzi wako? Jibu lilikuwa vifuatavyo:

Wengi walisema kwamba lugha ya Kiswahili aghalabu haitumiwi.

**Jedwali la 3.9: Majibu Kutokana na Kipengee cha Lugha Inayotumiwa Kanisani**

| Jumla | Nambari chanya | % chanya | Nambari hasi | % hasi |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 33 | 82.50 | 7 | 17.50 |

Kutokana na yaliyomo katika jedwali hili, asilimia 82.50 wanakubaliana ya kwamba lugha ya Kiswahili haitumiwi katika kuendeleza mahubiri makanisani na jambo hili ni kikwamizi katika kufanikisha mwingiliano kati ya Kiswahili na Kijaluo.

### 3.2.9 Viongozi

Kutokana na utafiti uliofanya katika jimbo dogo la Marindi, hakuna hata mwalimu mkuu mmoja aliyekiri kutumia lugha ya Kiswahili. Nilipowauliza kusema kama ni lugha ipi wanayowashawishi wanafunzi wao kuitumia,wote walikiri kwamba ni lugha ya Kiingereza. Watatu walikiri kutokuwa na programu za kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili shuleni mwao.

Mahojiano yaliyofanywa ana kwa ana yalikuwa;

9. Je, unazitumia lugha zipi katika mawasiliano yako baina ya wanafunzi wako na hata walimu?

Kiswahili na Kiingereza ☐

Kiingereza ☐

Kiswahili tu ☐

10) Je, unawashawishi wanafunzi wako kutumia lugha ipi/zipi?

Kiswahili ☐

Kiingereza ☐

Kiingereza na Kiswahili ☐

Wengi wa walimu walikosa vifaa kama vya kufunzia lugha hii ya Kiswahili. Jambo hili lilionyesha kutojali kwa wale wakuu wa shule hasa kufungamana na swala la vifaa vya kufunzia lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 3.10: Majibu Kutokana na Kipengee cha Viongozi**

| Jumla | Chanya | % Chanya | Hasi | % Hasi |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 28 | 70% | 12 | 30% |

Kutokana na utafiti huu asilimia 70 ya walengwa walikiri kwamba viongozi si kielelezo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili katika eneo hili. Asilimia 30 walikiri kwamba viongozi wengine hutumia lugha hii.

### 3.2.10 Hadhi

Walengwa wengi walionyesha mitazamo hasi kuihusu lugha hii ya Kiswahili. Kupitia kwa mahojiano pamoja na hojaji, wengi wao walikuwa na sababu zao za kutoienzi lugha hii ya Kiswahili. Walengwa wengi (63.5) walihoji kuwa matumizi ya Kiswahili hayaendani na hadhi kama yalivyo yale ya Kiingereza Marindi.

**Jedwalila 3.11: Majibu Kutokana na Kipengee cha Hadhi**

| Walengwa | Jumla | Chanya | % Chanya | Hasi | % Hasi |
|---|---|---|---|---|---|
| Walimu wa Kiswahili | 8 | 8 | 100 | 0 | 0 |
| Walimu wakuu | 4 | 0 | 0 | 4 | 100 |
| Wanafunzi | 10 | 2 | 20 | 8 | 80 |
| Wazazi | 8 | 3 | 37.5 | 5 | 63.5 |

Jedwali hili limetumiwa hivi ili kubainisha mitazamo ya kila kikundi. Kwa mfano, walimu wote 8 wa shule zote wanaienzi lugha ya Kiswahili.Kwa upande mwingine, walimu wakuu wote wana mitazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Wanafunzi kwa upande wao wana mitazamo hasi kuihusu lugha ya Kiswahili wakionyesha mapendeleo kwa lugha za Kiingereza na Sheng'. Wazazi nao si vielelezo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa maana wenyewe hawaifahamu.

### 3.2.11 Ajira

Swala hili la ajira lilizua changamoto sana hasa kwa walimu kwani, walipojibu swali la 18, yaani;

> 18) Ni changamoto zipi umeweza kukumbana nazo katika kuifunza na kujifunza lugha ya Kiswahili?

Wengi wa walimu watafitiwa walijibu kwamba wanakosa motisha katika kufunza. Wanafunzi pia waliweza kutaja changamoto wanazokumbana nazo katika kufunzwa lugha.Walimu wakuu pia walikuwa vikwamizi.Walimu wote, kupitia kwa walimu wakuu.

Waliipigia debe matumizi ya Kiingereza. Japo lugha ya Kijaluo ilipigwa marufuku kutumiwa shuleni, walimu walijikuta wakitumia lugha hii baina yao au hata kuwasiliana na wafanyikazi wengine au hata wanafunzi.Hii ni kwa sababu walimu takribani wote wa shule zinazotafitiwa wanatoka vijiji vya karibu na shule.

**Jedwali la 3.12: Majibu Kutokana na Kipengee cha Ajira**

| Jumla | Nambari Chanya | % Chanya | Nambari Hasi | % Hasi |
|---|---|---|---|---|
| 40 | 20 | 50 | 20 | 50 |

Jambo hili la ajira lilikuwa na asilimia sawa. Kuna wale waliosema ajira sio kipengee muhimu katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na kunao pia waliosema kinyume. Wale walioona Kiswahili kama nyenzo ya ajira walirejelea walimu wa Kiswahili ilhali wale waliopinga waliona namna Kiingereza kilienziwa katika nchi jirani ya Tanzania.


### 3.3 Muhtasari wa Vipengele Visivyohusu Lugha

Muhtasari wa vipengele hivi visivyo vya lugha vimeelezwa hapo chini kwa kutumia grafu. Kuna jumla ya watafitiwa chanya na vile vile watafitiwa hasi.

**Jedwali la 3.13: Majibu Kutokana na Vipengele Visivyohusu Lugha**

| | **Chanya** | **Hasi** |
|---|---|---|
| Umbali wa kijamii | 16 | 24 |
| Tofauti za kiumri | 24 | 16 |
| Tofauti za vipaji | 23 | 17 |
| Motisha | 35 | 5 |
| Elimu | 15 | 25 |
| Kushawishika na marika | 25 | 15 |
| Lugha inayotumika makanisani | 33 | 7 |

**Chati ya 3.1: Majibu Kutokana na Vipengele Visivyohusu Lugha**




Wengi wa watafitiwa walionyesha kupitia kwa majibu yao kwamba mitazamo yao kuhusiana na lugha ya Kiswahili iliathiriwa kwa kiasi kikubwa na vipengee visivyohusiana na lugha. Watafitiwa 33 kwa mfano, walikiri kuitumia Kijaluo katika


mawasiliano yao makanisani.Watafitiwa 35 kwa 40 kwa upande mwingine walikipa kipaumbele kipengele cha motisha.Kwa hivyo,walidhihirisha yale mawazo ya Lambert na Gardner (1972) ambao wanasisitiza kipengee cha motisha katika kujifunza lugha ya pili.

Nadharia ya Saikolojia ya Jamii ilitumika katika uchanganuzi wa data katika utafiti huu. Ni nadharia inayohusu vipengele ambavyo hutuongoza ili tuwe na tabia fulani hasa tulipo na wenzetu na huchunguza masharti ambayo husababisha tabia fulani au hata hisia fulani (Lambert na Gardner 1972).

### 3.3.1 Uchanganuzi wa Walengwa

Katika kuchanganua data, kwanza nilichanganua watafitiwa kwa kutumia pai chati au umbo la duara.

**Chati ya 3.2: Uchanganuzi wa Walengwa**



**Jedwali la 3.14: Mitazamo ya Watafitiwa**


Tunapochanganua mitazamo ya watafitiwa hawa kwa kuzingatia asilimia, tunapata ya kwamba;

| | **Watafitiwa** | **Asilimia %** | **Digrii** |
|---|---|---|---|
| Walimu wakuu | 4 | 10 | 36 |
| Walimu wa kiswahili | 8 | 20 | 72 |
| Wanafunzi wa darasa la sita | 10 | 25 | 90 |
| Wanafunzi wa darasa la saba | 10 | 25 | 90 |
| Wazazi | 8 | 20 | 72 |
| Jumla | 40 | 100 | 360 |

### 3.3.2 Umbali wa Kijamii

Kutokana na data tulioueleza hapo juu, ilidhihirika wazi kuwa jinsi ilivyoelezwa katika 3.2.2 kulikuwa na umbali wa kijamii kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa watafitiwa wa Kijaluo.Jambo hili lilisababisha mitazamo hasi miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kijaluo. Kati ya walengwa 40, 15 tu ndio walionyesha shauku katika lugha ya Kiswahili. Wengine 25 walikuwa na mitazamo hasi. Wakati wa majadiliano na watafitiwa hawa, hawakuhisi mvuto wowote katika lugha hii ya Kiswahili.


**Chati ya 3.3 Uchanganuzi wa Umbali wa Kijamii**




### 3.3.3 Tofauti za Kiumri

Wengi wa wanafunzi walionyesha ustadi mwingi katika matumizi yao ya Kiswahili hasa tunapozingatia matamshi na lafudhi. Walimu wakuu walionyesha hali ya juu kuhusu umilisi lakini sio utendaji. Kwa upande mwingine wazazi walikosa umilisi na vilevile utendaji ingawa wengine wao walijaribu.

**Chati ya 3.4: Uchanganuzi wa Kipengee cha Tofauti za Kiumri**





### 3.3.4Tofauti za Vipaji

Kutokana na maelezo ya utafiti katika 3.2.4, watu wazima walikosa uwezo wa kuwa na vipaji vya hali ya juu katika Kiswahili. Sababu zenyewe zilikuwa kwamba

mitazamo yao ilikuwa hasi. Kwa hivyo, ili kujifunza lugha iliwabidi kuwa na mitazamo chanya, motisha na maelekezo ya mazingira ili kufaulu katika kuwa na vipaji vya juu,(Lambert 1963).


**Chati ya 3.4:Uchanganuzi wa Kipengee cha Tofauti za Vipaji**




### 3.3.5Motisha

Walengwa walibaini ya kwamba kipengee cha motisha ni kipengee muhimu katika miingiliano ya lugha. Kwa mujibu wa Lambert na Gardner (1972) ikiwa wazungumzaji wanataka aidha kupanda ngazi kijamii au kufaidi utamaduni, ingewabidi kujifunza lugha ngeni. Na ili kuwa na ufanisi, lazima kuwe na motisha katika jimbo hili dogo.Kutokana na utafiti huu, wakazi wa Marindi hawajapewa motisha ili waweze kuwa na ufanisi katika kujifunza Kiswahili.

**Chati ya 3.5: Uchanganuzi wa Kipengee cha Motisha**




Kama inavyojidhihirisha kwenye paichati hii,kipengele cha motisha katika kujifunza Kiswahili Marindi chavutia digrii 315,kumaanisha motisha ni kipengee muhimu.

**3.3.6 Elimu**


Katika eneo la Marindi Kaunti ya Migori, lugha hii ya taifa imesusiwa kama inavyoonyeshwakupitia kwa utafiti uliofanywa. Wengi wa wakazi wa Marindi wana mitazamo hasi.Kuhusu Kiswahili, asilimia 62.5 wana mitazamo hasi ilhali 37.5 wana mitazamo chanya. Mitazamo hii inaweza kudhihirisha ya kwamba;

1. Jamii hii ya Wajaluo hawataki kujitambulisha na lugha hiiya Kiswahili.
2. Wajaluo wana dhana potovu na mitazamo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili.
3. Wajaluo wachache wanaoitumia lugha hii wana matumizi duni kwa hivyo sio vielelezo kwa wengine kwenye suala la ujifunzaji wa lugha hii ya Kiswahili.
4. Watu wa Marindi hawaionei fahari lugha yenyewe ya Kiswahili.

5. Watu wa Marindi wameathiriwa na lugha nyingine kama vile lugha ya mama na Kiingereza.

6. Watu wa Marindi hawajaweza kuipa hadhi inayofaa lugha ya Kiswahili.

**Chati ya 3.6:Uchanganuzi wa Kipengee cha Elimu**





### 3.3.7 Kushawishiwa na Marika

Mazingira ni lazima yawe mema ili wanafunzi waweze kuwa na ufanisi katika kujifunza lugha yoyote ile. Kwa mujibu wa Bunting (2004) mazingira ya ujifunzaji lugha yana athari kwa mitazamo ya wanafunzi kwa ujumla.

Kutokana na waliyoyasema watafitiwa, wameathiriwa na lugha ya Sheng' au lugha ya mama na lugha ambayo inatumiwa na marika zao. Majibu kutokana na utafiti wetu ni kwamba, asilimia 62.50 wameathiriwa na marika ilhali asilimia 37.5 hawajaathiriwakatika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Wengi wa walengwa ambao wameathiriwa na marika labda hawaoni umuhimu wowote katika kujifunza lugha sanifu ya Kiswahili.Hii ni kwa sababu ile dhana "sisi" kinyume na "wao" inaelekea kuwa muhimu sana kwao inapokuja kwenye suala la lugha katika mawasiliano.


**Chati ya 3.7: Uchanganuzi wa wa Kipengee cha Kushawishiwa na Marika**




### 3.3.8Lugha Inayotumika Kanisani

Kutokana na matokea ya huu utafiti, lugha ya Kijaluo ndiyo hutumiwa katika kuendeleza mahubiri makanisani, katika sala, katika matangazo na vile vile katika nyimbo za kumsifia Mungu. Asilimia 82.5 ambayo imewakilishwa na digrii 297 wana mitazamo hasi kuhusu Kiswahili na hawaitumii lugha yenyewe wakiwa kanisani. Asilimia 17.5 ya watafitiwa ndio hutumia lugha hii.

**Chati ya 3.8: Uchanganuzi waKipengee cha Lugha Inayotumika Kanisani**




### 3.3.9 Viongozi

Kupitia kwa utafiti huu,yaliyojidhihirisha katika kipengee hiki ni kwamba kipengee cha viongozi huathiri mitazamo kuhusu Kiswahili kwa kiwango cha juu. Kwa mfano, walimu wakuu kama viongozi wa shule hawana programu za kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili na pia hawawapi walimu wao wa Kiswahili vifaa kama vile kamusi za semi,kamusi za methali,kamusi za vitendawili, vitabu vya mashairi na vya insha pamoja na magazeti ya Taifa Leo.Wanafunzi pia hawapewi majarida ya ngeli ili kuweza kuimarisha matumizi yao ya lugha kwani ngeli ndio uti wa mgongo wa lugha hii ya Kiswahili. Jambo hili limethibitisha mitazamo yao kuhusu Kiswahili. Yafuatayo yafaa kufanywa na viongozi ili kuimarisha ukuzaji wa Kiswahili.

1. Viongozi wote wanapaswa kuwa vielelezo vya ujifunzaji wa Kiswahili popote walipo.
2. Kaunti ya Migori ina wakazi kutoka sehemu zote za dunia kwa hivyo lugha inayotumiwa inapaswa kuwa ya taifa.Hivyo basi, viongozi wafaa kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika eneo hili la Marindi,na Kaunti ya Migori kwa jumla.
3. Lugha inayotumika katika mikutano shuleni, kanisani na kwingineko si lugha ya taifa ambayo ni kinyume na hali inavyofaa kuwa.

**Chati ya 3.9: Uchanganuzi wa Kipengee cha Viongozi**



### 3.3.10 Hadhi

Walengwa wengi walionyesha mitazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Wanafunzi walikuwa na sababu za kukizira Kiswahili zifuatazo kupitia kwenye hojaji zao;


1. Hawakuwa na vitabu vya kutosha vya kiada, na vile ambavyo vilikuwa havikuwatosha.
2. Hawakuwa na vitabu vya hadithi kwa Kiswahili.
3. Wazazi hawakuwanunulia kamusi kwa hivyo, ilikuwa vigumu kujifunza lugha ya Kiswahili kivyao.
4. Hawakupewa insha za Kiswahili za kutosha.
5. Mazoezi ya Kiswahili darasani hayakusahihishwa.
6. Walimu wao wa Kiswahili hawakuelewa ngeli.
7. Walishauriwa kutumia lugha ya Kiingereza. Wengi wa wanafunzi walitumia lugha yao ya mama.
8. Walimu walikosa kuhudhuria masomo yao ya Kiswahili.

**Walimu kwa upande mwingine;**

1. Walilalamikia madarasa yenye wanafunzi wengi kupita kiasi.
2. Walimu wenzao hawakuienzi lugha ya Kiswahili kwa hivyo, ilikuwa nadra kutumiwa kwenye chumba chao.
3. Hawakuhudhuria kozi zozote ambazo zingeimarisha matumizi yao ya lugha ya Kiswahili.

Wazazi walijitetea kwa kusema wanakosa kuwa vielelezo kwa vile hawakuielewa lugha ya Kiswahili.Jambo hili ndilo lilisababisha mitazamo hasi ya lugha ya Kiswahili.


**Chati ya 3.10: Uchanganuzi wa Kipengee cha Hadhi**




### 3.3.11 Ajira

Kwa kuzingatia miingiliano kati ya lugha ya Kijaluo na Kiswahili, twapata ya kwamba inaathiriwa na suala hili la ajira. Lugha ya Kiswahili inapaswa kutumiwa kazini, katika mawasiliano. Asilimia 50 ya watafitiwa walitumia lugha ya Kiswahili ilhali asilimia nyingine 50 walitumia Kijaluo makazini. Sababu ya hali hii ni kwamba kuna Waluhya, Wakisii na wengineo katika jimbo hilo.Kwa hivyo, wazungumzaji wasio Wajaluo hutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao ilhali wale wengine kutumia lugha yao ya asili.

**Chati ya 3.11: Uchanganuzi wa Kipengee cha Ajira**



### 3.3.12 Hitimisho

Kulingana na jinsi data ilivyowasilishwa na kuchanganuliwa, kuna vipengee visivyohusika na lugha ambavyo huathiri mitazamo ya lugha. Kwa jumla vipengee hivi vikitiliwa maanane na wazungumzaji wowote wale wa lugha hii mitazamo kuhusu lugha ya Kiswahili itakuwa chanya.

1. Wazungumzaji wajaribu kuwaiga wale wenye vipaji vya juu katika lugha ya Kiswahili ili kuzua mitazamo chanya ya lugha ya Kiswahili.
2. Wazungumzaji wowote hasa wa lugha ya pili huhitaji motisha ili kupata ufanisi katika matumizi ya lugha hiyo husika. Hali hii inaweza kutumikizwa kwa Kiswahili katika jimbo hili dogo la Marindi na katika Kaunti nzima ya Migori kwa jumla.
3. Lugha ya Kiswahili lazima itambuliwe kama lugha ya taifa na ipewe hadhi yake kwa njia inayofaa.

Sura hii imebainisha mitazamo waliyo nayo wanafunzi, walimu pamoja na wazazi kuhusu Kiswahili katika Kaunti ya Migori nchini Kenya. Katika sura ifuatayo, na ambayo ndiyo ya mwisho, tunatoa muhtasari wa mahitimisho na vile vile mapendekezo kwa tafiti za baadaye kuhusiana na mada yetu ya utafiti.

# SURA YA NNE

## MATOKEO YA UTAFITI

### 4.1 Utangulizi

Katika sura ya 3 niliwasilisha data kuhusiana na mada ya utafiti na kuichanganua. Katika sura hii nitawasilisha matokeo yanayotokana na ule uchanganuzi wa data ili kudhihirisha mambo ambayo husababisha mitazamo hasi na athari za mwingiliano katika matumizi ya Kiswahili katika eneo la Marindi katika Kaunti ya Migori.

Kutokana na uchanganuzi wa data tuliofanya katika sura ya 3, inabainika kwamba yapo masiala yanayojitokeza na kusababisha mitazamo ama hasi au chanya au hata horomo dhidi ya matumizi ya Kiswahili Marindi. Kwa kutaja vipengee visivyohusiana na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, moja baada ya nyingine, tutajadili matokeo.

### 4.2 Umbali wa Kijamii

Matokeo ya mitihani katika lugha ya Kiswahili katika jimbo hili hayajawa ya kutia moyo. Katika utafiti huu na hasa katika mahojiano baina yangu na walimu wakuu, ni shule moja tu ndio iliyokuwa na matokeo ya kuridhisha kidogo katika Kiswahili.
Sababu za kutoridhisha kwa matokeo nilizozipata ni kwamba wanafunzi ni wengi katika madarasa yao. Katika shule mbili wanafunzi walikuwa zaidi ya 60 katika darasa moja. Nilipomhoji mmoja wa walimu wakuu, aliyesema matokeo ya mitihani yamekuwa mazuri katika shule yake kwa muda. Hivyo basi wazazi huwapeleka watoto wao kwa wingi pale. Mwalimu mkuu mwingine naye alisema wazazi huwalazimisha watoto wao kurudia madarasa katika shule yake. Jambo ambalo anashindwa kuepukana nalo kwa sababu ya sera ya elimu nchini Kenya.

Kutokana na wanafunzi waliofurika madarasani, walimu na wazazi walikiri ya kwamba ni vigumu kupata vifaa vya kuwatosha wale wanafunzi wote. Bila shaka, wanafunzi wanapofurika hivi darasani, wanakosa ule mvuto kwa vile vifaa vyenyewe havitoshi; jambo ambalo husababisha umbali wa kisaikolojia na vile vile umbali wa kijamii baina yao na wazungumzaji wa jamii - lugha lengwa na katika muktadha huu Kiswahili. Miingiliano yao hupungua (Schumann,1978a). Upungufu huu husababishwa na umbali wa kijamii.

Jambo jingine ambalo liliweza kudhihirika wazi ni kwamba tafiti hazifanywi kwa wingi katika shule hizi. Na hata ikiwa tafiti zenyewe zinafanywa, watafiti wenyewe hawachukui muda wao ili kwenda kujadiliana na walengwa kwa kuwapa matokeo ya tafiti zao. Jambo hili hufanya wengi wa walengwa kuwa na mitazamo hasi na wengine hata kukataa kuziregesha hojaji. Ni bayana kutokana na utafiti wangu kuwa, Wajaluo hawataki kujitambulisha na lugha hii ya Kiswahili kwa sababu ya umbali wa kijamii baina ya Wanailoti na Wabantu.

### 4.3 Tofauti za Kiumri

Kutokana na utafiti uliofanywa, hata ikiwa wazungumzaji wanajifunza lugha ya pili hawatimizi malengo asili. Lazima wawe wanaathiriwa na mambo mbalimbali. Kwa mfano, kuna vipengee tambuzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Watu wazima wanapojifunza lugha ya pili na hata ya kigeni, huzingatia kanuni za isimu ilhali watoto hutumia lugha kwa kuzingatia maana yake (Ellis, 1985). Mwanafunzi hawi na mitazamo tofauti tofauti kati ya lugha moja na nyingine. Watu wazima huwa na mitazamo tofauti tofauti kuhusu lugha yao wenyewe pamoja na lugha lengwa. Utambuzi huu ni ule unaoletwa na umri. Jambo ambalo hufanya vijana kujifunza lugha kwa urahisi zaidi kuliko watu wazima ni hali yao ya kumbukumbu (Rosansky

1975). Wazazi wana uwezo wa kuathiri mazungumzo ya watoto kwani, watoto hao huwaiga. Ugumu na makosa mengi yanayopatikana katika lugha ya pili hutokana na athari za lugha ya kwanza (Lee, 1968). Katika muktadha wa wakazi wa eneo la Marindi katika Kaunti ya Migori ni Wajaluo na kwa hiyo athari za watu wazima huweza kuwafikia watoto au watu wa umri mdogo vile vile.

## 4.4 Tofauti za Vipaji

Walimu huathiri kipengee hiki cha vipaji kwa kiasi kikubwa. Kutokana na utafiti, wengi wa walimu wa Kiswahili walidai kuwa na masomo mengi mno. Jambo hili limewaathiri wanafunzi kwasababu hawapewi mazoezi ya kutosha, hasa katika insha. Na hata wanapopewa, wanafunzi wamezua changamoto kwamba aghalabu insha zao hazisahihishwi kwa wakati ufaao na kisha kukawa na mjadala kuzihusu. Hii ni kumaanisha kwamba, ikiwa wanafunzi wamefurika katika madarasa yao, mwalimu hana uwezo wa kuwashughulikia wanafunzi wake kibinafsi. Mara nyingi watashughulikia wale ambao wanafanya vyema na kutojali wenye vipaji vya chini. Bila motisha wanafunzi na vile vile walimu watakosa ufanisi katika kujifunza na kufunza lugha yoyote ile ikiwemo lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo washika dau wote wana jukumu hasa katika ufanisi wa wanafunzi katika lugha hii ya Kiswahili.

## 4.5 Motisha

Walimu waliohojiwa walisema kwamba hawajishughulishi na mambo yoyote ya kitaaluma kama vile kusahihisha mitihani ya kitaifa na hata kuhudhuria warsha mbalimbali za Kiswahili. Kuna wale ambao wameajiriwa hivi maajuzi kwa hivyo hawana uzoefu wa kutosha. Hawa ni wale ambao walipatikana katika viwango vya miaka kati ya 0-5ya ufunzaji na wengine wakawa na masomo mengi kupita kiasi.

Walimu na wanafunzi katika eneo la Marindi wanakuwa na mitazamo hasi katika lugha hii ya Kiswahili kwa sababu ya kukosa vifaa. Vifaa vyenyewe kama vile vitabu havitoshi, na vile ambavyo vinapatikana, wanafunzi wale hugawa baina ya hata wanafunzi wanne. Kwa hivyo wanapopewa mazoezi ya ziada, wengi wao hawayakamilishi. Jambo ambalo linawakosesha walimu na wanafunzi wao motisha.

Katika utafiti huu wanafunzi wanaathiriwa na mazingira yao. Kuna shule ambazo madarasa yake yalikuwa hayana madirisha. Kwa hivyo wanafunzi walikuwa wanaathiriwa na hali ya anga kama vile mvua au baridi kali. Katika sura ya pili nilijadili jambo kuhusu nafasi. Earthman, (2004) anaeleza ya kwamba ubora wa mazingira ya mwanafunzi huathiri uwezo wake na jinsi anavyojifunza. Kwa kutumikiza fikira hizi za Earthman, inaonekana kwamba mazingira ya Marindi yanahasiri ujifunzaji wa Kiswahili katika eneo hili la Migori.

**4.6 Elimu**

Katika utafiti wangu, wengi wa walimu hawakupendezwa na mitindo ya uongozi pale shuleni, kwani mwalimu mkuu alijiamulia mambo mengi kwa mfano kuhusu vitabu vilivyonunuliwa. Walimu wa Kiswahili hawakuwa na vitabu vya hadithi kwa hivyo wanafunzi wao walishindwa kuimarisha lugha ya Kiswahili.

Walimu wengine wasio wa Kiswahili pamoja na walimu wakuu hawakuchangia sera ya lugha kuhusu matumizi ya Kiswahili katika shule zao. Wwalimu wakuu walikiri katika hojaji kwamba huzungumza kwa kutumia Kiingereza na lugha ya mama. Jambo hili lilifanya matokeo ya lugha ya Kiswahili yadorore katika shule zenye walimu wakuu sampuli hii. Mwanafunzi anapopokea lugha ya pili, na kwa muktadha huu Kiswahili, wanaelimishwa.

## 4.7 Kushawishiwa na Marika

Wengi wa wanafunzi walitumia lugha ya Sheng, Kiingereza na lugha ya mama ya Kijaluo. Kiswahili kilipewa kisogo. Kuna walimu ambao walikuwa na umri wa kati ya miaka 25-30 ambao walikiri kuzitumia lugha mbili; Kiingereza na Kiswahili. Katika majadiliano yao walisema kwamba wakiwa nje ya darasa wao huweza kutumia lugha ya Sheng`. Kwa hivyo wengi wao huathiriwa na marika wakazitumia lugha ambazo hupendelewa zaidi na marika zao.

## 4.8. Lugha Inayotumika Kanisani

Jimbo dogo la Marindi lililoko katika Kaunti ya Migori lina wakazi wanaozungumza lugha tofauti tofauti ila, wanajimbo hili hususia kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao wakiwa makanisani. Kwa kutumia kinasa sauti, niliweza kunasa mahubiri katika kanisa moja lililoko katika jimbo hilo. Nyimbo huwa katika lugha ya mama, vile vile sala. Mara moja moja tafsiri hufanywa kutoka lugha hiyo ya Kijaluo hadi Kiswahili. Kwa hivyo lugha ya Kijaluo hupewa kipaumbele kuliko lugha ya Kiswahili.Kwa kuifunza lugha ya Kiswahili katika masuala ya Kiungu, mielekeo ya wakazi wa Marindi dhidi ya Kiswahili vilevile hujitokeza kuwa hasi.

## 4.9 Viongozi

Kutokana na utafiti wangu katika shule nne, nilipata kwamba viongozi wote walikuwa wa kiume. Wote walikiri kwamba hawatumii lugha ya Kiswahili wakiwa shuleni, kwa mfano katika mikutano au hata kwenye gwaride. Walionekana kusahau kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa inayofaa kuenziwa.

## 4.10 Hadhi

Lugha hii ya Kiswahili ilionekana kukosa hadhi kubwa ikilinganishwa na lugha ya mama pamoja na Kiingereza. Haya yalielezwa katika sura ya 3.

## 4.11 Ajira

Kati ya walimu wale wanane, wawili walikuwa na shahada ilhali wengine walikuwa walimu wa P1. Walimu walio na uzoefu wa juu husaidia sana katika kuinua viwango vya elimu katika shule na jamii kwa jumla.

## 4.12 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, inaeleweka kwamba wanafunzi, wazazi na walimu wana mitazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Pia inadhihirika kwamba kuna vikwamizi ambavyo husababisha matokeo duni dhidi ya Kiswahili.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Baada ya matokeo, nitajadili muhtasari wa mambo ambayo yanachangia kwa mitazamo hasi kwa Kiswahili miongoni mwa Wajaluo na athari zake.

### 5.2 Muhtasari

Matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika jimbo hili hayaridhishi kwa sababu;

1. Wanafunzi hufurika madarasani na walimu kushindwa kushugulikia kila mmoja wao.
2. Kwa kuwa si walimu wengi wenye asili ya Kijaluo wanaopenda Kiswahili, wanaofunza wanatwikwa jukumu la masomo mengi kupita kiasi, hivyo basi aghalabu hufanya kazi duni.
3. Watafitiwa wameathiriwa na lugha nyingi kama vile Kiingereza na Kijaluo kwani hawataki kujitambulisha na lugha hii ya Kiswahili.
4. Walimu wachache wa Kijaluo katika eneo hili la Marindi, wanakosa motisha katika kazi zao hivi kwamba hakuna tofauti baina yao na wengine. Wanapaswa kuwa vielelezo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili ili wale wengine ambao wana mitazamo hasi waibadilishe mitazamo yao.
5. Walimu wakuu katika eneo la Marindi wana mitazamo hasi ya lugha ya Kiswahili. Wakiwa mstari wa mbele katika kuvuvia tanuu ya maendeleo ya Kiswahili katika eneo hili, wataibadilisha mitazamo ya wengi. Hii ni kwa sababu wanatumia lugha ya Kiingereza kwa wingi na hata mara nyingine hutumia hata Kijaluo wakiwa katika miktadha rasmi.
6. Wazazi katika eneo la Marindi wanatumia lugha ya mama ya Kijaluo, kila mara wakiwa nyumbani na watoto wao. Mitazamo yao ni hasi hivi kwamba

wazazi hawa huwaathiri watoto wao. Vile vile hawashughuliki kuwapa vifaa vinavyohitajika kama vile magazeti ya Taifa Leo na Kamusi.

7. Mazingira yameathiri vijana kwani wanaionea fahari lugha ya Sheng`. Lugha hii ya Sheng' inazua hali ya kubadilisha msimbo wakati wa mawasiliano.
8. Walimu na wanafunzi wa Kiswahili wamekosa vifaa vya kutosha vya kufunzia na kujifunzia lugha ya Kiswahili.

### 5.3 Hitimisho

Kiswahili kimepewa jukumu la kuwa lugha rasmi na vile vile kuwa lugha ya taifa nchini Kenya. Wazazi wanapaswa kufanya kila jitihada ili kuwa vielelezo katika ujifunzaji wa Kiswahili, kwa watoto wao, hasa wakiwa nao manyumbani. Wazazi wanapaswa kuienzi lugha hii ya Kiswahili kwa kuwasiliana na watoto wao na hata kuwasaidia katika mazoezi yao wakiwa nyumbani. Pia, wanapaswa kuwanunulia watoto wao vifaa vya kutumia shuleni. Wanafunzi wengi wanalalamika kwamba hawanunuliwi vifaa kama kamusi na hata vitabu vya kiada.

Walimu wa Kiswahili kwa upande mwingine, wanapaswa kuwajibika katika ufunzaji wa lugha ya pili. Wengi wao wanakiri kuwa na mitazamo chanya kuhusu lugha hii ya Kiswahili kwa hivyo, wanapaswa kujitolea mhanga kuwasaida wanafunzi wao katika lugha ya Kiswahili. Wanapewa masomo mengi kupita kiasi. Walimu wenzao pamoja na mwalimu mkuu wanasusia kutumia lugha hii ya Kiswahili. Aghalabu wanafunzi hutumia lugha ya mama ya Kijaluo ambayo huwafanya walimu wale wa Kiswahili wafe moyo.

Walimu wakuu hawatumii lugha hii ya Kiswahili, wakiwa shuleni kwa mfano wakiwa kwenye diskosi rasmi kama vile, mikutano na hata wanapotoa hotuba zao wakiwa gwarideni. Walimu hawa wakuu hawanunui vifaa kama vile, vitabu vya kiada

vinavyohitajika pamoja na vitabu vya hadithi. Madarasa mengi shuleni hayana madirisha, jambo ambalo linawaathiri wanafunzi. Pia, lugha inayotumika katika kumbukumbu za mikutano na ripoti katika batli za shule, haziandikwi kwa lugha ya Kiswahili.

## 5.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, pamoja na mahitimisho kuhusu lugha ya Kiswahili, mapendekezo ni kama ifuatavyo;

1. Juhudi lazima ziwekwe na wakuu wa shule, Wizara ya Elimu na washika dau kwa jumla, ili vifaa vya kufunzia na kujifunza lugha ya Kiswahili viwe vya kutosha, kama vile madarasa yanayofaa kwa wanafunzi. Jambo hili kuhusu vifaa litainua kipengee cha motisha kwa wanafunzi na walimu wanaojifunza na kufunza lugha ya Kiswahili.
2. Walimu wa Kiswahili lazima wawe na mazoea ya kuhudhuria kozi za kunoa ubongo pamoja na warsha ili wajipige msasa kuhusu mbinu wanazozitumia na kuwa vielelezo katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika Kaunti ya Migori.
3. Wakuu wa shule Marindi, lazima wahakikisha ya kwamba sera za shule ambazo zimekubaliwa kutumika, zinatumika kwa usawa. Sera hizi zitazuia kupendelewa au kutopendelewa kwa lugha nyingine, katika muktadha wowote wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.
4. Mandhari ya shule kilugha katika Kaunti ya Migori, yasionyeshe upendeleo wowote wa lugha moja dhidi ya nyingine kwa mfano, lugha inayotumiwa katika mabango shuleni, katika kutajia madarasa na ofisi na hata lugha katika wito wa shule.

5. Mwingiliano kuhusu lugha baina ya mwalimu wa shule na mwalimu mkuu wake, baina ya mwalimu wa Kiswahili na mwalimu mwenzake, na baina ya mwalimu wa Kiswahili na wazazi ukiwa chanya, bila shaka maingiliano ya wanafunzi wakiwa shuleni yatakuwa chanya.
6. Mwisho, wazungumzaji wa Kijaluo waipe lugha ya Kiswahili hadhi inayofaa.Jamii hii ya Wajaluo haijaelewa uzuri wa kufanya utafiti kwani,wana mitazamo hasi kuhusu watafiti hasa wanaotafiti kwa lugha ya Kiswahili. Katika Kaunti hii ya Migori, watafitiwa wanauona kama mzigo mkubwa kuzijaza hojaji na kuziregesha. Wakiwa na mitazamo chanya kuzihusu tafiti hasa za Kiswahili, watasaidia katika kuinua viwango vya elimu hasa katika somo la Kiswahili katika eneo la Marindi, Kaunti ya Migori kwa jumla.

# MAREJELEO


Allwright, D.et al (1991). *Focus on the Language Classroom*, New York: Cambridge University Press.

Allwright, R.L. (1990). *What Do You Want Teaching Materials For? Currents in Language Teaching*. Oxford: Oxford University Press.

Baker, C. (2001). *Foundation of Bilingual Education and Bilingualism* (3rd) ed. Cleredon: Multilingual Matters.

Brown, C. (1985). *Requests for Specific Language Input*: *Differences Between Older and Younger Adult Language Learners* In Gass and Madden (eds.).

Brown, H. (1980). *The Optimal Distance Model on Second Language Acquisition:* TESOL Quarterly 14: 157-64.

Buliba, A.et al (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*; Nairobi: J.K.F.

Bunting, A. (2004). *Secondary Schools Designed for a Purpose*: *But which One*? Teacher, No. 154 pp. 10-13.

Burstall, C. (1975). *Factors Affecting Foreign Language Learning*: *A Consideration of Some Relevant Findings: Language Teaching and Linguistics.* Abstracts 8:5-125).

Caroll, R. (1987). *Two Approaches for Investigation of Second Language Acquisition in Context in Ellis* (ed.). Rowley, Mass: Newbury House.

Chomsky, C. (1969). *The Acquisition of Syntax in Children from 5 to 10. Cambridge:* Mass MIT Press.

Cohen, A. (1999). *Strategies to Learning and Using A Second Language.* London: Longmann.

Cook, V. (1991). *Second Language Learning and Language Teaching.* London: Edward Arnold 169 pp.

Culp, B. (2005). *Management of the Physical Environment in the Classroom and Gymnasium: It is not that different teaching Elementary Physical Education* Vol. 17 No. 5 pp.

Dana, S. (2009). *Research Methods for Social Psychology.* Hongkong: Fabulous Pte Ltd.

Earthman, G.I. (2004). *Prioritization of 31 Criteria for School Building.* Adequacy: American Civil Liberties Union Foundation of Maryland Assessed online on 30/04/07 at <http://www.actomd.org.

Ellis, R. (1985). *Understanding Second Language Acquisition.* Oxford: Oxford University Press.

_________(1994). *The Study of Second Language Acquisition.* Oxford: Oxford University Press.

Eysenck et al(1964). *Manual of the Eysenck Personality.* London; University of London Press.

Fillmore, W. (1982). *Instructional Language as Linguistics Input*: Second Language Learning in Classrooms. Wilkinston, New York: Academic Press.

Gardner, R. (1979). *Social Psychological Aspects of Second Language Acquisition* in H. Giles and R. St.Claid (eds) Language and Social Psychology. Oxford: Basil Blackwell.

__________ (1980). *On the Validity of Affective Acquisition in Second Language Acquisition: Conceptual Contextual and Statistical Considerations and Statistical Considerations Language Learning* 30: 255 – 70.

Gardner,R.C et al. (1972). *Attitudes and Motivation in Second Language Learning.* Rowley, Mass: Newbury House.

Halliday, M (1973). *Explorations in the Functions of Language*. London: Edward Arnold.

Higgins. et al, (2005). *The Impact of School Environment: A Literature Review*. The Centre of Learning and Teaching School of Education Science. University of Newcastle.

Hockett, C.F. (1958). *A Course in Modern Linguistics*. New York; Macmillan.

Hudson, R.A (1980). *Sociolinguistics.* Australia: Cambridge University Press.

*Katiba ya Kenya*. Sura ya 2, Ibara ya 7, Sehemu ya 1.

Kimaro, H. (2010, Juni, 29) *Lugha ina Majukumu kwa Jamii*, Gazeti la Taifa Leo Uk. 16.

Krashen, S. (1982). *Principles and Practices in Second Language Acquisition.* London: Pergamon.

Lahey, B.B. (2011). *Essentials of Psychology of Bilingualism*. Journal of Social Issues 23: 91.

Lee, W. (1968). *Thoughts on Contrastive Linguistics in One Context of Language Teaching* in J. Alatis (ed.).

Lightbrown, P.et al, (1999). *How Languages are Learnt* (Rev. ed) Oxford; England: Oxford University Press.

Long. M et, (1983). *Classroom Foreigner Talk Discourse*: *Forms and Functions of Teachers Questions* In H. Seliger & M. Long (Eds.) *Classroom Oriented Research in Second Language*, *Acquisition* pp (268-285). Rowley, M.A: Newbury House.

Marton, W. (1981). *Contrastive Analysis in the Classroom In Frisiak* (ed.) 1981.

Mbara, J.A. (2010). *The Attitude of Suba Youth towards the Suba Language. A Case Study of Kaksingri, Tasnifu ya Uzamili ambayo Haijachapishwa*, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Meenkashi H.V. (2008). *Learners' Attitudes and its Impact on Language Learning. Uttar Pradesh*, I.I. E & T.

Mowrer, O. (1960). *Learning Theory and Symbolic Processes*. New York: John Wiley and Sons.

Mugenda, O. et al, (2003). *Research Methods Qualitative and Quantitative Approaches Nairobi*: Acts Press.

Mukhwana, A. (2008). *Language Attitude in Urban Kenya: A Case Study of Nairobi, Kisumu na Mombasa*, Tasnifu ya Uzamifu PhD), Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Neufeld, G. (1978) "*A Theoritical Perspective in the Nature of Linguistic Aptitude International Review of Applied Linguistics*: ix 115-23.

Obura, A.P. (1982). *Attitudes and Motivation Language Learning Strategies and Achievement in French in Kenya Secondary Schools*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ogero, J.O. (2008). *Institution Based Factors Influencing Students Performance in Kiswahili at KCSE in Public Schools* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Oller, J.et al (1978). *A Further Comment on the Language Proficiency as a Source of Variance in Certain Affective Measures – Language Learning* 28:417-23

Osgood, C. et al, (1957). *The Measurement of Meaning*. United States: University of Illinois Press.

Oso, W. et al, (2008). *A General Guide to Writing Research Proposal and Report*: Kampala: Makerere University.

Owiyo,W.(2013). *The Impact of Interaction between Mother-tongue and Kiswahili: Philosophical Analysis of performance of Kenya Certificate of Primary Education*, Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Owong`a, Y. et al, (2010 Machi 16). *Pendekezo Sheng` Iharamishwe Lugha Isiwe Hiari*. Gazeti la Taifa Leo, uk.15.

Rosansky. E. (1975). *Methods and Morphenes in Second Language Acquisition*: Language Learning 26: 409-25.

Rosenthal et al, (1968). *Pygmation in the Classroom:Teacher Expectations and Pupils Intellectual Development*. New York: Holt; Rinehart na Winston. P. 209.

Rubin, J. (1975). *What the "Global Language Learner Can Teach Us*. "TESOL Quaterly 9/1.

Savington, S. (1991). *Communicative Language. Teaching. State of the Art* TESOL Quarterly 25/2 261-277.

Schiffman, H.R. (1976). *Sensation and Perception An Integrated Approach* New York: Wiley.

Schumann, J. (1978a). *The Pidginization Process. A Model for Second Language Acqusition.* Rowley Mass: New Hypothesis in Hatch (ed.) 1978a.

Skehan, P. (1989) *Individual Differences in Second Language Learning* London: Edward Arnold.

Stern, H. (1983). *Fundamental Concepts of Language Teaching Oxford*: Oxford University Press.

Tarone, E. (1983). *On The Variability of Interlanguage Systems. Applied Lingusitics* 412 143-63.Wilkenson (ed) New York: Academic Press.

Tesser, A. (1983) *Social Psychological Bulletin.*

UNESCO (1953). *The Use of Venacular Languages In Education. Monographs on Foundations of Education, No 8.* Paris: UNESCO.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO CHA KWANZA

## BARUA YA KUJITAMBULISHA KWA WATAFITIWA

**JAEL A. OWALA**

**S.L.P. 438**

**SUNA-MIGORI**

TAREHE

Kwa Bi./ Bwana,____________________________________________

KUH: MITAZAMO KUHUSU KISWAHILI MIONGONI MWA WAZUNGUMZAJI WA KIJALUO KIFANI CHA SHULE ZA MSINGI KATIKA KAUNTI YA MIGORI.

Mimi ni mwanafunzi wa Uzamili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi. Ninafanya utafiti kuhusu mada iliyotajwa hapo juu. Naomba unisaidia kujaza hojaji zilizounganishwa na barua hii, kwa uaminifu.

Nakuahidi ya kwamba majibu yako pamoja na utambulisho wako utakuwa wa siri mno. Habari nitakazozipokea kutoka kwa hojaji zenyewe zitatimika tu katika utafiti wangu.

Shukrani kwa ushirikiano wako.

Wako mwaminifu,

**JAEL AKINYI OWALA**

## KIAMBATISHO CHA PILI

## HOJAJI KWA WALIMU WAKUU

Kwa Bi./Bwana,_____________________________________________.

Huu ni utafiti unaochunguza vikwamizi vinavyochangia matokeo duni ya mitihani katika kaunti ya Migori.

Tafadhali yajibu maswali yote kwa kutoa majibu mwafaka, ukizingatia maswali uliyoulizwa. Habari nitakazozipokea kutoka kwa hojaji zitakuwa za siri mno. Ushirikiano wako utakuwa wa manufaa.

1. Jina la shule yako ni?____________________________________________

2. Aina ya shule ni ya?

   Wasichana pekee ☐ wavulana pekee ☐

   Mchanyanyiko ☐

3. Unawalimu wangapi wa Kiswahili katika shule yako? ___________________

4. Wamehitimu vipi kitaaluma?

   P 1 ☐ Shahada ☐ Diploma ☐

5. Je, shule yako imefaulu vipi katika mitihani ya kitaifa ya Kiswahili kwa miaka mitano iliyopita, jinsi ilivyoandikwa hapa chini?

| Mwaka | Alama wastani |
|---|---|
| 2013 | |
| 2012 | |
| 2011 | |
| 2010 | |
| 2009 | |

6. Sababu za matokeo haya kuwa zilivyo zaweza kuwa zipi?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

7. Walimu wako wanafaulu vipi katika ufunzaji wa somo hili la Kiswahili?______________________________________

______________________________________________

8. Je wanafunzi wako nao wanafaulu vipi katika somo hili la Kiswahili? Kadiria.

Wastani ☐ Stadi ☐ Duni ☐

9. Unawasiliana na wanafunzi au walimu wako kwa lugha gani?

Kiswahili na Kiingereza ☐

Kiingereza tu ☐

Lugha ya mama ☐

10. Je, unawahimiza wanafunzi wako kuitimia lugha ipi/zipi wakiwa shuleni?

Kiswahili ☐

Kiingereza ☐

Kiingereza na Kiswahili ☐

11. Wanafunzi wako wanapendelea lugha gani wanapowasiliana wenyewe kwa wenyewe?Na kwa nini?

Kiingereza na Kiswahili ☐

Kiswahili ☐

Kiingereza ☐

Lugha ya mama ☐

Sheng` ☐

12. Mna maktaba?

Ndio ☐ Hapana ☐

13. Ikiwa ndio, mna nunua vitabu vya hadithi za Kiswahili?

Ndio ☐ Hapana ☐

14. Madarasa yako yana wanafunzi wangapi katika kila darasa?

Darasa la 6 ☐ Darasa la 7 ☐

15. Je, maoni yako ni yapi kuhusu nambari ya wanafunzi katika kila darasa na matokeo kuhusu Kiswahili? Yanaathirika vipi?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

16. Unakumbana na changamoto zipi hasa katika somo hili la Kiswahili?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

17. Kwa maoni yako ni mikakati ipi unayoweza kutumia ili kuboresha matokeo katika shule yako hasa kuhusiana na somo la Kiswahili?

______________________________________________

______________________________________________

18. Shule yako inamaprogramu ambayo walimu wa Kiswahili hujiimarisha kwayo katika lugha hii?

Ndio ☐ Hapana ☐

19. Lugha gani hutumiwa katika kanisa lenu? Unaweza kusema kuwa lugha hii ina athari zozote kwa wanafunzi wako?

________________________________________

________________________________________

*Shukrani kwa ushirikiano wako.*

## KIAMBATISHO CHA TATU

## HOJAJI KWA WALIMU

Tafadhali tia alama [ √ ] ama andika jibu lako kwenye pengo lililoachwa wazi. Habari tutakazopata katika hojaji hii zitakuwa za siri. Ushirikiano wako utakuwa wa manufaa kwangu. Tafadhali usiandike jina lako.1. Eleza jinsia yako.

Mke ☐ Mume ☐

2. Tia alama [ √ ] kwenye umri wako.

Chini ya miaka 25 ☐

Kati ya miaka 25 – 30 ☐

Kati ya miaka 30 – 39 ☐

Zaidi ya 40 ☐

3. Hali yako ya kuhitimu kitaaluma ni ipi ?

P1 ☐

Stashahada/ Diploma ☐

Shahada ☐

Mengine (elezea zaidi)________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

4. Umeifunza lugha ya Kiswahili kwa miaka mingapi?

0-5 ☐ 6-10 ☐ 11-16 ☐ Zaidi ya 16 ☐

5. Una masomo mangapi kwa wiki?________________________________

6. Masomo yako mengine ni?____________________________________

7. Darasa lako lina wanafunzi wangapi? ______________________________

8. Unajishughulisha na mambo mengine ya kitaalamu kama vile, kusahihisha mitihani ya kitaifa na warsha mbali mbali kuhusiana na lugha ya Kiswahili?

Ndio ☐ Hapana ☐

Eleza zaidi kuhusu jibu lako. ______________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

9. Je, mna vitabu vyote vinavyohitajika vya kiada pamoja na vya hadithi za Kiswahili?

Ndio ☐ Hapana ☐

10. Hii ni orodha ya vifaa vinavyohitajika katika kufunza na kujifunza Kiswahili katika shule ya msingi. Tia [ √ ] kwa vifaa vinavyopatikana na [ x ] kwa vile ambavyo havipatikani

| VIFAA | KUPATIKANA | KUTOPATIKANA |
|---|---|---|
| Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI) | | |
| Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Karne ya 21). | | |
| Kiswahili Mufti Darasa la 6 (Toleo Jipya). | | |
| Kiswahili Mufti Darasa la 7 (Toleo Jipya). | | |
| Kiswahili kwa Darasa la 6. | | |
| Kiswahili kwa Darasa la 7. | | |
| Kamusi ya Methali. | | |
| Kamusi ya Semi na Nahau. | | |

| | | |
|---|---|---|
| Kamusi ya Vitendawili. | | |
| Hatua kwa Hatua Kwa darasa la 6. | | |
| Hatua kwa Hatua Kwa darasa la 7. | | |
| Vitabu vya hadithi. | | |
| Vitabu vya Mashairi. | | |
| Vitabu vya insha. | | |
| Magazeti ya Taifa Leo. | | |
| Majarida ya ngeli za majina ya Kiswahili. | | |

11. Vipengee vifuatavyo ni vikwamizi katika kufunza na kujifunza kwa lugha ya Kiswahili. Onyesha ikiwa vipengee hivyo huathiri matokeo ya Kiswahili katika shule yenu.

a)Vifaa shuleni kama vile madarasa Ndio ☐ La ☐

b)Mtindo wa kuendesha shule Ndio ☐ La ☐

c)Nyenzo za kufunza na kujifunza Ndio ☐ La ☐

12. Je, wewe hutoa mazoezi ya ziada ya Kiswahili mara ngapi?

Kila siku ☐ Kila wiki ☐ Kila baada ya wiki mbili ☐

13. Unatumia lugha gani katika mawasiliano yako na wanafunzi wako?

Kiswahili pekee ☐

Kiingereza na Kiswahili ☐

Kiingereza ☐

14. Aghalabu wanafunzi hutumia lugha ipi au zipi wakiwa shuleni?

Kiswahili pekee ☐

Kiswahili na kiingereza ☐

Kiingereza ☐

15. Kwa kukadiria, kiwango cha wanafunzi wako katika Kiswahili ni kipi?:-

Stadi ☐ Wastani ☐ Viwango vya chini ☐

16. Sheng' imewaathiri ujifunzaji wa Kiswahili wa wanafunzi wako kwa njia yoyote?

Ndio ☐ La ☐

17. Una athari zozote za lugha ya asili unapofundisha Kiswahili?

Ndio ☐ La ☐

18. Ni changamoto zipi ambazo umeweza kukumbana nazo katika kuifunza na kujifunza lugha ya Kiswahili?

______________________________________________

______________________________________________

19. Je, mawazo yako ni yapi kwa waunda sera ili kuimarisha viwango vya elimu hasa ukijikita katika lugha ya Kiswahili?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

20. Kipengee cha motisha ni suala muhimu katika ufunzaji wa lugha ikiwemo ile ya Kiswahili?.

Ndio ☐ Hapana ☐

***Nashukuru kwa ushirikiano wako.***

## KIAMBATISHO CHA NNE

## MASWALI YA VIWANGO KWA WALIMU WA KISWAHILI

Tafadhali piga mviringo (o) katika taarifa uliyopewa hapo chini ukionyesha kwamba;

Nakubaliana kabisa (1)

Nakubaliana (2)

Nina shaka (3)

Nakataa kabisa (4)

1. Silabasi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa darasa la 6/7 ni pana zaidi.

   1 2 3 4

2. Silabasi hii haiwezi kukamilishwa kwa urahisi kwa kuzingatia muda unaoratibiwa.

   1 2 3 4

3. Napenda kuifunza lugha hii ya Kiswahili.

   1 2 3 4

4. Nina ugumu katika kusahihisha Insha za Kiswahili.

   1 2 3 4

5. Siwezi kupeana mazoezi mengi kwa sababu wanafunzi ni wengi madarasani.

   1 2 3 4

6. Walimu wa Kiswahili lazima wahudhurie warsha,ili waweze kuimarisha lugha ya Kiswahili.

   1 2 3 4

7. Wanafunzi wangu wana motisha katika kujifunza lugha hii ya Kiswahili.

1 2 3 4

8. Lugha ya Kiswahili ina manufaa katika maisha kwa jumla.

1 2 3 4

9. Lugha hii ya Kiswahili hutumika shuleni wakati wote.

1 2 3 4

10. Naridhishwa na matokeo katika mitihani ya wanafunzi wangu hasa katika somo la Kiswahili.

1 2 3 4

## KIAMBATISHO CHA TANO.

## HOJAJI KWA WANAFUNZI

Tafadhali tia alama [√] ama andika jibu lako kwenye pengo lililiachwa wazi. Habari tutakazopata katika hojaji hii zitakuwa za siri.

Usiliandike jina lako.

1. Eleza jinsia yako.

   Msichana [ ]   Mvulana [ ]

2. Darasa lako ni lipi?

   Sita [ ]   Saba [ ]

3. Lugha unayoienzi kabisa ni ipi?

   Kiswahili [ ]   Kiingereza [ ]   Sheng' [ ]

4. Je, unaipenda lugha ya Kiswahili?

   Ndio [ ]   Hapana [ ]

5. Je, mwalimu wako wa Kiswahili anakuridhisha na hali yake ya kufunza?

   Ndio [ ]   Hapana [ ]

6. Mnapewa mazoezi ya ziada kwa muda upi ?

   Kila siku [ ]

   Kila wiki [ ]

   Kila wiki mbili [ ]

   Hatupewi [ ]

7. Ikiwa mnapewa mazoezi, yanasahihishwa?

   Ndio [ ]   Wakati mwingine [ ]

   Hapana [ ]

8. Je, mwalimu wenu hukubali kuulizwa maswali au kutoa michango katika somo lake la Kiswahili?

Ndio ☐ Hapana ☐

. Wewe huzitumia lugha zipi ukiwa shuleni?

Kiswahili na kiingereza ☐

Kiingereza tu ☐

Kiswahili tu ☐

Sheng' ☐

Lugha ya asili/ mama ☐

10. Je, mwaka huu umesoma vitabu vya hadithi ngapi?

Hakuna ☐ 1-2 ☐ 3-4 ☐ Zaidi ya 5 ☐

11. Katika shule yenu kuna vitabu vya kutosha vya Kiswahili?

Ndio ☐ Hapana ☐

12. Darasa lenu limewahi kukosa mwalimu wa Kiswahili kwa muda?

Ndio ☐ Hapana ☐

13. Ikiwa ndio, kwa muda upi?

Masomo 1 – 3 ☐

Wiki 1-2 ☐

Muhula 1 ☐

14. Je, mwalimu wenu huwa na masomo ya ziada anapokosa kuyahudhuria masomo yake?

Ndio ☐ Hapana ☐

15. Una shida zipi kama mwanafunzi wa Kiswahili katika kujifunza lugha hii ?

16. Mawazo yako ni yapi katika kuinua viwango vya somo la Kiswahili katika shule yenu?

17. Wanafunzi wote ambao wamefanya vizuri katika mitihani hupewa zawadi? Ni kwa nini?

*Shukrani kwa ushirikiano wako.*

## KIAMBATISHO CHA SITA

## MASWALI YA VIWANGO KWA WANAFUNZI

Tafadhali piga mviringo (o) katika taarifa uliyopewa hapo chini ukionyesha kwamba;

Nakubaliana kabisa (1)

Nakubaliana (2)

Nina shaka (3)

Nakataa kabisa (4)

1. Naipenda sana somo la Kiswahili.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

2. Kiswahili ni kigumu mno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

3. Napenda kuziandika insha za Kiswahili.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

4. Naitumia lugha hii ya Kiswahili katika mawasiliano na wenzangu nikiwa shuleni.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

5. Lugha ya Kiswahili ina manufaa,kwangu kama mwanafunzi wa Kiswahili.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

6. Mitihani ya Kiswahili ni migumu mno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

7. Siridhishi na jinsi mwalimu wetu wa Kiswahili huifunza lugha hii ya Kiswahili.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

8. Matokeo yangu ya mitihani katika lugha ya Kiswahili ni ya kuridhisha.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

9. Ninapata muda wa kusoma vitabu vya hadithi katika lugha ya Kiswahilinikiwa shuleni.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

10. Napenda kusoma gazeti la Taifa Leo na kusikiliza vipindi vya Kiswahili redioni.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 |

## KIAMBATISHO CHA SABA

## HOJAJI KWA WAZAZI

### UTANGULIZI

Habari tutakazopata katika hojaji hii zitakuwa za siri. Tafadhali jibu maswali yote ukifuata maagizo. Tafadhali tia alama [√] ama andika jibu lako kwenye pengo lililoachwa wazi.

1. Eleza jinsia yako Mke ☐ Mume ☐

2. Wewe ni mkaazi wa eneo la Marindi?

   Ndio ☐ Hapana ☐

3. Umri wako ni kati ya miaka ipi?

   18-25 ☐ 26-35 ☐

4. Je, umeajiriwa?

   Ndio ☐ Hapana ☐

5. Je, umeolewa?

   Ndio ☐ Hapana ☐

6. Tafadhali eleza kiwango chako cha elimu.

   ..........................................................................................

   ..........................................................................................

7. Je, unazungumza lugha zipi?

..............................................................................................

..............................................................................................

8. Kati ya lugha ulizotaja, unazungumza lugha ipi na familia yako?

..............................................................................................

..............................................................................................

9. Ukiwa kazini, wewe hutumia lugha gani?

..............................................................................................

..............................................................................................

10. Unatumia lugha yako ya kiasili wakati gani?

..............................................................................................

..............................................................................................

11. Maoni yako ni yapi kuhusu lugha ya Kiasili?

..............................................................................................

..............................................................................................

12. Unahisi vipi unapotumia lugha hii ya Kiasili?

..............................................................................................

..............................................................................................

13. Maoni yako ni yapi kuhusu Kiswahili?

..............................................................................................

..............................................................................................

14. Unahisi vipi unapotumia lugha hii ya Kiswahili?

..............................................................................................

..............................................................................................

15. Una ufahamu wowote kuhusu mitazamo kuhusu Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Dholuo?

Ndio ☐ Hapana ☐

16. Mitazamo kuhusu Kiswahili katika eneo hili ni:

Chanya ☐

Hasi ☐

17. Ikiwa mitazamo hii ni hasi, ulitambua vipi?

..........................................................................................

..........................................................................................

.................

18. Mwelekeo wako ni upi kuhusu lugha ya Kiswahili?

Chanya ☐ Hasi ☐

19. Eleza kuhusu matokeo ya mitihani katika eneo hili la Marindi katika lugha ya Kiswahili.

..........................................................................................

..........................................................................................

20. Ni sababu zipi zinazozua matokeo duni ya mitihani ya Kiswahili katika eneo hili la Marindi?

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

**Maswali ya Viwango**

Tafadhali piga mviringo (O) katika taarifa uliyopewa hapo chini ukionyesha kwamba;

1. Ninakubaliana kabisa.
2. Ninakubaliana.
3. Sikubaliani kabisa.
4. Sikubaliani.
5. Sina maoni.

1. Maoni yako ni yapi kuhusu lugha ya Kiswahili?

   1 2 3

2. Kiswahili ni lugha inayostahili kutumika katika mawasiliano yetu ya kila siku.

   1 2 3 4 5

3. Kiswahili inafahamika kama lugha ya Wabantu, kwa hivyo ni wao tu wanaopaswa kuitumia lugha hiyo ya Kiswahili.

   1 2 3 4 5

4. Kiswahili ni lugha inayotumiwa na watu wenye viwango vya chini vya elimu.

   1 2 3 4 5

5. Lugha hii ya Kiswahili hutumia sana katika makazi yetu.

   1 2 3 4 5

6. Ni walimu wa Kiswahili tu katika jimbo hili dogo ndio la Marindi wana uwezo wa kuzungumza lugha hii ya Kiswahili kwa ufasaha.

   1 2 3 4 5

7. Wafanyibiashara katika jimbo hili dogo la Marindindio hutumia lugha ya Kiswahili, katika kuziendeleza biashara zao.

   1 2 3 4 5

8. Viongozi wetu ni kielelezo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili katika jimbo hili.

1 2 3 4 5

9. Lugha hii ya Kiswahili hutumiwa katika jimbo hili dogo la Marindi kuendeleza mahubiri makanisani.

1 2 3 4 5

10. Lugha hii ya Kiswahili hutumiwa katika mikutano yote shuleni.

1 2 3 4 5

11. Lugha hii ya Kiswahili hutazamwa kama ile ya wazee na sio ya vijana.

1 2 3 4 5

12. Motisha ina umuhimu katika kuamua kufaulu au kutofaulu katika muktadha wowote wa kujifunza lugha.

1 2 3 4 5

13. Ujuzi wa lugha hii ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa hutegemea vipaji vya mzungumzaji.

1 2 3 4 5

14. Mwingiliano kati ya walimu na wazazi na wazazi katika lugha ya Kiswahili ni wa kutamausha.

1 2 3 4 5

15. Mwingiliano kati ya wazazi na wanafunzi katika lugha ya Kiswahili ni wa kutamausha

1 2 3 4 5

## KIAMBATISHO CHA NANE

## RATIBAYA WAKATI

## 2014

| KAZI | FEB | MACHI | APRILI | MEI | JUNI | JULAI | AGOSTI | SEPT | OCT | NOV |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mada iliyoteuliwa kwa utafiti | ■ | | | | | | | | | |
| Utafiti kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada | | ■ | | | | | | | | |
| Kuandika pendekezo la utafiti | | | ■ | | | | | | | |
| Kuwasilisha pendekezo la utafiti kwa idara | | | | ■ | | | | | | |
| Kukusanya data | | | | | ■ | | | | | |
| Kuwasilisha na kuchanganua data | | | | | | ■ | | | | |
| Kuwasilisha mswada wa kwanza wa tasnifu | | | | | | | ■ | | | |
| Marekebisho ya mswada | | | | | | | | ■ | | |
| Kuwasilisha nakala tatu za tasnifu zilizounganishwa | | | | | | | | | ■ | |
| Utetezi wa tasnifu | | | | | | | | | | ■ |
| Wasilisho la mwisho la tasnifu zilizounganishwa | | | | | | | | | | ■ |

**KIAMBATISHO CHA TISA**

**BAJETI YA TASNIFU**

| MAELEZO | GHARAMA(SH) |
|---|---|
| 1.**UCHAPISHAJI WA KAZI** | |
| Kununua tarakilishi | 40,000 |
| Kuchapisha pendakezo (nakala ya kwanza) | 1,500 |
| Marekebisho ya pili ya pendekezo | 2,000 |
| Marekebisho ya tatu ya pendekezo | 2,000 |
| Kuchapisha ripoti ya mwisho ya pendekezo. | 2,000 |
| Kuchapisha hojaji | 3,000 |
| 2.**VIFAA VYA KUANDIKA** | |
| Vifaa vya kuandikia | 1,000 |
| Karatasi za kurudufia | 1,500 |
| Kalamu vifutio, penseli | 200 |
| 3.**USAFIRI** | |
| Kupeana hojaji | 1,000 |
| Kushauriana na wasimamizi | 30,000 |
| 4. **KUUNGANISHA KAZI** | |
| Kuunganisha pendekezo nakala 3. | 1,000 |
| Kuunganisha ripoti ya mwisho ya tasnifu (nakala 8) | 10,000 |
| 5.**ANUWAI** | 15,000 |
| **JUMLA** | **110,200** |